SportPesa
CHEZA USHINDE SASA
SPORTPESA.CO.TZ | PIGA *150*87#
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa



**Wafungwa** 5,704 wasamehewa na Rais Samia

UKURASA 7




**Mbappe azipasua kichwa PSG, Madrid**

UKURASA 22

Nipashe
Jumanne Desemba 28, 2021 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
ISSN 0856 • Na. 0580808
www.ippmedia.com
MWANGA WA JAMII
www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US

# Nabii Mwingira kuhojiwa Polisi



• **Yatoa** saa ishirini na nne... *Endelea ukurasa 2*

Waziri Simbachawene

Nabii Mwingira

## Kaburi lafukuliwa jeneza lavunjwa mwili watelekezwa

UKURASA 5

## Chanjo UVIKO-19 nyumba kwa nyumba

UKURASA 2

**MICHEZO** NABI ATAJA SIKU YA UBINGWA UK.24 | MAONI, KATUNI UK.6

# Nabii Mwingira kuhojiwa

**Na Elizabeth Zaya**

WAZIRI wa Mambo ya Ndani, George Simbachawene, ameliagiza Jeshi la Polisi Kanda Maalumu ya Dar es Salaam, kumtafuta na kumhoji Nabii wa Kanisa la Efatha, Josephath Mwingira, kuhusu shutuma mbalimbali alizozitoa wakati akihubiri siku ya Sikukuu ya Krismasi kanisani kwake, Mwenge, jijini Dar es Salaam.

Miongoni mwa shutuma anazodaiwa kuzitoa ni pamoja na kutishiwa maisha mara kadhaa.

Akijibu swali baada ya kuulizwa na waandishi wa habari jana jijini Dar es Salaam kuhusu tuhuma hizo alizozitoa Mwingira, Waziri Simbachawene alisema ameona shutuma hizo kupitia mitandao ya kijamii na kuahidi kulishughulikia suala hilo.

"Hili nimelisikia siku hizi mbili za Sikukuu ya Krisimasi la nabii Mwingira kwenye mitandao, nimepata ile 'clip' (kipande cha video) ni tuhuma nzito hasa linapotolewa na kiongozi wa kijamii wa dini na maarufu anayejulikana, bado tunaendelea kulifuatilia," alisema Waziri Simbachawene.

"Lakini kama alikuwa anapatwa na matukio yote yaliyokuwa yanatokea kama alivyodai, kwa nini alikuwa hatoi taarifa kwenye vyombo kama Jeshi la Polisi ili hatua zichukuliwe na kuwatafuta wahusika, mpaka asubiri Krisimasi ya mwaka 2021," alihoji na kuongeza;

"Kama aliyoyasema yatakuwa ni kweli tutahitaji atusaidie kutupa taarifa zaidi na kwa kuwa tunautafuta uhalisia, sio vibaya RPC wa Kanda Maalumu ya Dar es Salaam akamtafuta ili kupata ukweli zaidi kwa sababu pale kanisani alikuwa anaongea na waumini."

Waziri Simbachawene alisema kwa kuwa nchi inaongozwa na utawala wa haki na sheria, hakuna haja ya mtu kukaa na hofu na maisha yake.

"Nchi yetu inaongozwa na utawala wa haki na sheria, hakuna haja ya mtu kukaa akiwa na hofu na maisha yake, tunahitaji kuchukua maelezo yake ya kutosha ili kushughulika na hao aliowataja," alisisitiza Simbachawene.

**POLISI YATOA SAA 24**

Jeshi la Polisi Kanda Maalumu ya Dar es Salaam, imeagiza ndani ya saa 24 kuanza kuhojiwa kwa Nabii Mwingira, kuhusu tuhuma mbalimbali alizozitoa dhidi ya serikali, ikiwa njama za maofisa wa serikali kutaka kumuua.

"Jeshi la Polisi limefikia hatua hiyo baada ya kufuatilia kwa kauli zinazodaiwa kutolewa na Askofu (Nabii) huyo na kuona kama zinajenga hofu na chuki kwa wananchi dhidi ya serikali yao," Muliro Muliro, Kamanda wa Polisi Kanda Maalum ya Dar es Salaam alisema.

"Kwa uzito wa mambo yanayodaiwa kutolewa na Askofu (Nabii) huyo ni lazima apatikane haraka iwezekanavyo na ahojiwe kwa kina juu ya kila kipengele ambavyo Jeshi linaona kuna viaashiria vya vigezo vya jinai," alisema.



Waziri wa Mambo ya Ndani, George Simbachawene, akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana katangaza msamaha wa wafungwa zaidi ya 5000 waliopata msamaha uliotolewa na Rais, Samia Suluhu Hassan, katika maadhimisho ya Siku ya Uhuru. PICHA: JUMANNE

## Chanzo mauaji ya mama chatajwa

**Na Daniel Sabuni,** MERERANI

MFANYABIASHARA wa madini aina ya Tanzanite wa mkoani Arusha, Ruth Mmasy, anayedaiwa kuuawa na mwanawe na mwili wake kukutwa kwenye chemba ya choo, amezikwa jana huku mamia ya wanakijiji cha Mikungani, wilayani Arumeru, wakishiriki maziko hayo.

Chanzo cha mauaji hayo kimedaiwa kuwa ni tamaa ya mali.

Mchungaji wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzani (KKKT), Usharika wa Mikungani, Ernest Mola, akihubiri kwenye ibada ya mazishi hayo, alisema jamii wamesikitishwa na tukio hilo kwa kuwa marehemu alikuwa mtu wa kujitoa.

"Siku chache kabla ya uhai wake alichangia usharika Shilingi milioni moja, tukashukuru kwa namna alivyojitolea kwa Mungu," alisema mchungaji Mola.

Kaka wa marehemu Hamis Mmasy, alidai kuwa tamaa za mali ndizo zimesababisha, Patrick Mmasi (24) kumuua mama yake mzazi.

"Marehemu hakuwa anaumwa alikuwa mzima wa afya ndiyo hivyo kama ulivyosikia kuwa mtoto wake wa kumzaa mwenyewe amemuua mama yake," alisema Mmasy.

Mwenyekiti wa kijiji cha Mikungani, Mwalimu Issa Salum, alisema marehemu Ruth alisoma Shule ya Msingi Mikungani na alimfundisha kipindi alipokuwa mwalimu.

Mwenyekiti wa Mabkroka, Mkoa wa Arusha, Jeremia Simon, akisoma wasifu wa marehemu alisema, Ruth alizaliwa mwaka 1980 kwenye kitongoji cha Kairo mji mdogo wa Mirerani.

Simon alisema marehemu alipotea katika mazingira ya kutatanisha Desemba 11, mwaka huu na kugundulika amefariki Desemba 24 saa nane mchana Njiro Contena, jijini Arusha.

Rafiki wa marehemu huyo Jack Momo alisema wamesikitishwa kwa kuondokewa na rafiki yao katika kifo kilichosababishwa na mwanawe wa kumzaa.

# Chanjo UVIKO- 19 nyumba kwa nyumba

**Na Mary Geofrey,**
MKALAMA

MGANGA Mkuu wa Mkoa wa Singida, Dk. Victorina Ludovick, ameongoza Timu ya Uendeshaji na Usimamizi wa Huduma za Afya ya Halmashauri ya Mkalama kutoa elimu na chanjo ya UVIKO-19 nyumba kwa nyumba na mtaa kwa mtaa katika kufikia lengo la serikali la kuchanja wananchi 3,000 kila siku kwa mkoa huo.

Watalaamu hao walitumia njia ya miguu, kupita sehemu za biashara, mitaani, nyumbani na mashambani kuwapa elimu na kuwachanja wananchi waliokuwa tayari wilayani humo.

Wataalam hao wanatekeleza Kampeni ya Kuhamasisha na Utoaji wa Chanjo ya UVIKO-19, katika Mpango Shirikishi na Harakishi unaotekelezwa na Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, kupitia Kitengo cha Elimu ya Afya kwa Umma, inayoendelea nchi nzima.

Dk. Victorina akizungumza na watumishi hao kabla ya kuanza kuwatembelea wananchi, alisema lengo la kuchanja wananchi 3,000 kwa siku katika mkoa huo, litafikiwa kwa watumishi hao wa afya kutoka kwenye vituo vyao vya kazi na kuwafuata wananchi.

Aliwahimiza watumishi hao kutumia lugha rahisi inayoeleweka kwa jamii hiyo ili kupambana na maradhi hayo na kuisaidia serikali kufikia malengo yake iliyojiwekea ya kuchanja asilimia 60 ya Watanzania wote.

Naye, Mtaalam wa Ufuatiliaji na Udhibiti wa Magonjwa kutoka Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Baraka Nzobo, aliwahimiza wataalamu hao kuendelea kufanya kazi kwa ushirikiano ili kuongeza takwimu za uchanjaji.

Alisema mkoa huo upo nyuma katika takwimu za chanjo ya UVIKO-19 kwa sababu kubwa ya kukosekana kwa ushirikiano baina ya watumishi hao wa afya katika kutekeleza kampeni hiyo inayoendelea nchi nzima.

"Mnajisikiaje mnapoona mkoa wenu unashika mkia, takwimu za uchanjaji zipo chini na nyie mnaendelea kujivuta kuwafikia wananchi ni muhimu mkatimiza wajibu wenu," alisema Dk. Nzobo.

Wataalamu hao katika mitaa mbalimbali ya halmashauri hiyo' wakati wa kutoa chanjo, pia waliwahimiza wananchi kuendelea kuchukua tahadhari dhidi ya ugonjwa.

Wananchi nao walipata nafasi ya kuuliza maswali mbalimbali kabla ya kupata chanjo hiyo aina ya Pfizer ambayo inachomwa mara mbili baada ya siku 28.



Ofisa Elimu Sekondari wa Tanga jiji, Daudi Nchia akiongea na wanafunzi wa sayansi kutoka mikoa mbalimbali wakati wa uzinduzi wa kongamano la sita la sayansi lililofanyika katika kituo cha sayansi jijini Tanga jana. PICHA: HAMIDA KAMCHALLA

# Walalamika kukatwa malipo kwa kukosa mikataba

**Na Mwandishi wetu,** PEMBA

BAADHI ya wanachama wa kampuni ya Masterlife Kisiwani Pemba, wamelalamikia kukatwa fedha zao na wengine kutolipwa kabisa kutokana na kutokua na mikataba.

Walisema pamoja na kwamba hawakuwa na mikataba, lakini tayari walishafanyiwa uhakiki hapo awali na kuambiwa kwamba taarifa zao zipo katika kampuni hiyo na kuahidiwa ifikapo siku ya kurejeshewa fedha wanachama na wao watapatiwa haki zao.

"Zoezi la mwanzo ambalo tuliitwa na kufanyiwa uhakiki baada ya kutoa maelezo tulisajiliwa na taarifa zetu zilikubalika, lakini jambo la kushangaza baada ya kufika katika zoezi la urejeshewaji wa fedha tumetolewa bila kuangaliwa jambo hili limetuvunja moyo kwani hii ni haki yetu,"walisema waathirika hao.

Akizungumza na waandishi wa habari katika zoezi la urejeshaji fedha kwa wanachama hao, katika Kiwanda cha Makonyo Wawi Chake chake mwanachama ambaye hakutaka kutajwa jina lake alisema mkataba wake ulipotea na awali alipokwenda kwenye uhakiki alihakikiwa bila usumbufu wowote.

"Nilipohakikiwa nilisema mkataba wangu ulipotea na nikafanyiwa uhakiki vizuri tu nilionekana taarifa zangu lakini kwenye malipo niliposema umepotea nimeambiwa silipwi na hata kuniangalia jina langu kwenye kompyuta hawakutaka hii ni haki yangu kwanini wasinilipe,"alisema.

Alisema kiasi anachodai kupitia kampuni hiyo ni Sh. 500,000 ambazo aliziweka kwa mujibu wa mikataba waliyokubaliana na kampuni hiyo.

Mwanachama mwingine ambaye hakutaka kutajwa jina lake alisema baada ya milioni 6,000,000 ambazo aliziweka kupitia kampuni hiyo lakini alipewa milioni 3,170,000 na kwamba hakuna maelezo ambayo alipewa kuhusu ukatwaji wa fedha zake.

"Nataka kujua hizi pesa ambazo zimekatwa zimekwenda wapi na kama kuna tatizo kwanini serikali usituweke wazi tangu mapema tukajua tunalipwa kiasi gani lakini shida unapoingia ndani unakatwa pesa na hatupewi ufafanuzi," alisema.

Aidha, alimuomba Rais wa Zanzibar Dk. Hussein Mwinyi kulifuatilia tatizo hilo na kuwasikia kilio chao wanachama ambao fedha zao zimekatwa.

"Tunamuomba Rais wetu atusikie kupitia kilio chetu hiki ili tupatiwe haki zetu, mimi ni mnyonge hapa umenikata milioni 3,530,000 nitegemee kitu gani wakati ni haki yangu niliiweka kwa matumaini,"alisema.

Mwanachama Maryam Ramadhan alisema aliweka kiasi cha Sh. milioni 2,900,000 na makubaliano yao na kampuni ya Masterlife ni kuingiziwa faida jambo ambalo hata serikali ilielekeza wanachama wapewe fedha zao kamili lakini la kushangaza pesa zao zimekatwa.

"Pesa niliyoiweka mimi nilikubaliana na Masterlife waniingizie faida sijakubaliana nao kama baadaye waikate na serikali ilisema pesa zetu tutapewa kamili sasa tunachojiuliza hzizi pesa tunazokatwa zinakwenda wapi", alisema.

Kwa upande wake Kamishna wa Bajeti kutoka Ofisi ya Rais Fedha na Mipango Zanzibar, Saumu Khatib Haji alisema kwa Kisiwani Pemba wanachama takribani 230 wanatarajiwa kurejeshewa fedha zao kwa mujibu wa utaratibu.

Alisema kwa mwanachama ambaye jina lake limeonekana kwenye gazeti na halikuonekana katika matangazo yaliyobandikwa wataangalia katika kompyuta na ikiwa haki yake aliiweka na kuwa na vielelezo, atahudumiwa na kupatiwa fedha zake kwa mujibu wa utaratibu uliowekwa.

"Wale ambao fedha zao ni kidogo tunalipa kwa njia ya mkononi na mwenye kiwango kikubwa atalazimika kulipwa kupitia benki, changamoto zilizojitokeza ni upotevu wa mikataba ya wanachama, majina yapo lakini wanadai mikataba yao imeungua, imepotea lakini sisi tunawatambua kwani taarifa zao tunazo,"alisema.

Wanachama hao walilazimika kurejeshewa fedha zao baada ya kampuni hiyo kufungwa na serikali mwishoni mwa mwaka jana, kupitia Ofisi ya Rais Fedha na Mipango kufuatia agizo la Rais Mwinyi.


EAST AFRICAN CRUDE OIL PIPELINE

**MAOMBI YA TAARIFA YA KUONESHA NIA KWA AJILI YA UTOAJI WA UHANDISI WA HUDUMA ZA UGAVI WA MAJI KWA MRADI WA EACOP**
**KUMBUKUMBU NA. ECP-21-C-016**

KAMPUNI ya Mafuta na Gesi ya TOTAL East Africa Midstream BV (Company) Tanzania, inawaalika wakandarasi wazoefu na wanaoheshimika ambao wana uwezo unaoonekana, uzoefu uliothibitishwa, utayari na uwezo wa kueleza nia yao ya kutoa huduma zifuatazo kwa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki. mradi wa EACOP.

**MAELEZO MAFUPI YA UPEO WA HUDUMA:**
Uhandisi wa maji chini ya ardhi/mifumo yenye msingi wa visima na/au kuunganisha kwa mifumo iliyopo ya mtandao wa maji inajumuisha utafiti wa eneo-kazi, uchunguzi wa tovuti na Uhandisi wa kina. Upeo umefupishwa ndanimaelezoundani hapa chini

**Mifumo ya maji ya ardhini/kisima**
UFUNZO WA DESKTOP
Kusanya na kukagua nyaraka zozote zilizopo , ikijumuisha: 1/ tafiti za kijiofizikia na hidrojiolojia zilizofanywa mapema na Wizara ya Maji au taasisi nyingine yoyote; 2/ ramani zinazopatikana, picha za angani, ripoti na taarifa zingine za rasilimali maji za visima vilivyochimbwa hapo awali;
Fanya uchunguzi wa upelelezi eneo la ardhi pamoja na :
- hupitia njia za kijiolojia ili kutambua hali ya kijiolojia na hidrojiolojia
- Sensa ya visima vilivyopo, visima vyeye kina virefu, mikondo ya maji na vipengele vya maeneo yenye dalili za maji ndani ya eneo la kilomita 3 la kituo cha usambazaji kinachohitajika (SITE), au eneo linalopendekezwa la ukuzaji wa kisima ikiwa liko mbali na SITE;
- Upimaji wa visima vyeye kina virefu na visima vilivyopo, ikijumuisha kiwango cha maji na vipimo vya msingi vya ubora wa maji;

**Ripoti ikijumuisha**
- Ramani za Hydrojiolojia na Piezometric; ikijumuisha eneo na kina cha visima vilivyopo
- Utafiti wa dhana ya muundo wa kisima (inapowezekana kuifanya kutoka kwa utafiti wa eneo-kazi),
- Mpango wa program za ziada na kina wa uchunguzi unaohitajika kwa muundo wa kisima katika eneo husika.

**Tie-ins kwa mifumo iliyopo ya mtandao wa maji**
UFUNZO WA DESKTOP
Kusanya na kupitia takwimu zote muhimu kutoka katika mabonde yanayohusika na mamlaka za usambazaji maji kuhusu mtandao wa usambazaji maji uliopo, mfano ukubwa wa mabomba, vifaa vya ujenzi wa mabomba, ubora wa maji n.k.

**RIPOTI ikijumuisha:**
Uchambuzi wa data zote zilizokusanywa katika muktadha na uwezekano wa kuunganishwa kwa mitandao iliyopo ya usambazaji

**UCHUNGUZI WA ENEO**
Uchunguzi wa kijiofizikia kufanywa kwenye maeneo yanayoweza kuchaguliwa yaliyotambuliwa, mahsusi yaliyo chaguliwa na kpendekezwa ili kupata maeneo yenye maji. Ripoti ya uchunguzi wa itajumuisha:
- Programu ya uchunguzi na uhalali wa mbinu zilizochaguliwa za uchunguzi
- Ufafanuzi wa data, ikijumuisha: 1/Aquifer jiometri & sifa za majimaji na kuchaji upya, 2/kemia ya chemichemi na mambo yanayoathiri kemia; 3/ Uwezekano wa kuendeleza rasilimali za maji chini ya ardhi ikiwa ni pamoja na idadi inayotarajiwa ya visima, maeneo, kina, nk.

UBUNIFU WA KINA WA UHANDISI
- Ubunifu wa Kisima cha Maji, Bomba la Kisima cha Maji, Bomba, vifaa na vifaa vinavyozunguka, Hifadhi ya Maji,...
- Michoro ya kina, vipimo vya kiufundi

**UCHUNGUZI WA ENEO**
- Kutembelea maeneo ili kuimarisha mtandao uliopo katika eno husika kuzingatia eneo la kazi;
- Tathmini ya hali ya miundombinu iliyopo yaani hali ya bomba, pampu za nyongeza nk.
- Kuanzisha maeneo yanayowezekana kwa ajili ya kuunganisha;
- Sampuli na uchambuzi wa ubora wa maji
- Kufanya uchunguzi wa Topografia kwa njia za bomba
- Ripoti ya uchunguzi itakayo jumuisha taarifa pamoja na habari hapo juu

UBUNIFU WA KINA WA UHANDISI
- Kubuni mtandao kutoka eneo la mfumo mpaka eneo la kazi na pia kwa kuzingatia mifumo ya majumbani katika maeneo ya wananchi/jamii;
- Michoro ya kina, vipimo vya kiufundi

Kazi hiyo itafanywa katika maeneo mbalimbali nchini kote

**VIGEZO MUHIMU:**
Makampuni/Mashirika yanayoonyesha nia yanaalikwa kutuma maombi pamoja na nyaraka zifuatazo:
- Uthibitisho wa kusajiliwa na Brela ORS na CRB.
- Inashauriwa, mwonyesha nia atume maombi ya kusajiliwa katika kanzi data ya EWURA (LSSP) kama mtoaji na msambazaji wa huduma ndani ya nchi wakati wa kuwasilisha ombi la kuonesha nia.
- Kuzingatia Kanuni za maudhui ya Ndani za mwaka 2017 pamoja na tafsiri ya Kampuni ya Ndani na sheria za Kitaifa na Kimataifa pamoja na viwango vya Kimataifa vya mafuta na gesi.
- Maelezo ya uzoefu wa zamani katika kutoa uhandisi wa usambazaji wa maji: Uendelezaji wa kisima na/au kuunganishwa na mtandao uliopo wa maji.
- Orodha ya miradi iliyotangulia: maelezo, mteja, eneo,...
- Orodha ya vifaa na mifumo inayomilikiwa, wafanyikazi waliohitimu na wenye uzoefu
- Uthibitisho wa uwezo wa kifedha kutekeleza wigo uliopendekezwa wa huduma
- Maelezo ya mfumo wa afya usalama na mazingira na sera ya Ubora
- Nakala ya Sera za Kupambana na Rushwa na Maadili

Makampuni yenye nia, ambayo yana uwezo na rasilimali za kutoa huduma zilizotajwa hapo juu yanatakiwa kutuma taarifa ya kuonyesha nia iliyoandaliwa kwa lugha ya kiingereza pamoja na nyaraka tajwa kupitia barua pepe: **adeline.mmari@external.totalenergies.com** (ukubwa usiozidi MB20) hadi kufikia saa **9:00** mchana Majira ya Afrika Mashariki, tarehe **24 Januari 2022.** Kichwa cha Barua Pepe ni ECP-21-C-016/EOI.

**Muhimu:** Kwa ajili ya kutengeneza orodha ya makampuni ya Awali yenye vigezo, Mradi wa EACOP utapitia na kuchambua nyaraka zilizotumwa na makampuni yenye nia. Mwaliko kwa Makampuni kutuma maombi ya zabuni utatumwa kwa Makampuni ya Awali yenye vigezo baada ya makampuni hayo kusaini Makubaliano ya Utunzaji wa Taarifa (NDA).




Machinga wakiendelea na biashara zao katika eneo ambalo wameondolewa huku kukiwa na tangazo lenye ujumbe unaowazuia kuwapo, Mbezi Mwisho, Manispaa ya Ubungo Dar es Salaam juzi. PICHA: MPIGAPICHA WETU

# Samia akabidhi Bil. 12.1/- utekelezaji miradi maji

**Na Dotto Mwaibale,** SINGIDA

RAIS Samia Suluhu Hassan amekabidhi Sh. bilioni 12.1 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi mbalimbali inayolenga kupunguza kero ya maji kwa kiwango cha juu katika kipindi cha miezi sita kuanzia sasa kwa wananchi wa Mkoa wa Singida.

Hafla ya utiaji saini mikataba huo baina ya Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA) na wazabuni mbalimbali ilifanyika mkoani hapa mwishoni mwa wiki ikishuhudiwa na Mkuu wa mkoa huo, Dk. Binilith Mahenge na Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) mkoa wa Singida Juma Kilimba.

Meneja wa RUWASA mkoa wa Singida Mhandisi Lucas Japhary, alisema mikataba ya fedha hizo imegawanyika katika sehemu mbili, ya kwanza ni bajeti ya kawaida na pili ni fedha zinazotokana na miradi ya UVIKO-19.

“Kwa mwaka huu wa fedha tumetengewa fedha za miradi ya maji bilioni 12.1, na leo tunasaini mikataba ipatayo sita ya sehemu ya hiyo bajeti yenye thamani ya Sh. bilioni 3.9, lakini sehemu ya pili tutasaini mikataba ya fedha zinazotokana na UVIKO-19 ambayo kwa mkoa wetu wa Singida kwenye eneo la maji tumetengewa bilioni 4.9,” alisema Japhary.

Alisema katika fedha ya UVIKO wanatarajia kutumia Sh. bilioni 2.8 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maji mijini chini ya Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira mkoani hapa (SUWASA) kwa maeneo ya Singida Mjini, Manyoni na Kiomboi, huku kwa upande wa vijijini miradi mitatu inayotokana na fedha hiyo itakayohudumia vijiji sita yenye thamani ya Sh. bilioni 1.9 itakayosainiwa kwa maana ya kila mradi kwenda kuhudumu vijiji viwili.

Pia, Meneja huyo alimweleza Mkuu wa mkoa kuwa kukamilika kwa miradi hiyo tisa (kwa maana ya mitatu ya UVIKO na sita bajeti ya kawaida) ambayo inatarajia kukamilika ndani ya muda wa kipindi cha miezi sita kuanzia sasa inatarajia kupunguza kero kubwa ya maji kwa idadi ya wananchi zaidi ya laki tatu ndani ya Mkoa wa Singida.

Kwa upande wake, Mtendaji Mkuu wa SUWASA Mhandisi Patrick Nzamba, alisema kuhusu hali halisi ya utekelezaji wa miradi ya maji mijini kwa sasa tayari wameshasaini mkataba wa kusambaza mabomba wenye thamani ya Sh. milioni 244, pia mkataba mwingine ni ununuzi na usambazaji wa pampu zinazotarajiwa kufungwa kwenye chanzo cha eneo la Mwankoko na visima ndani ya manispaa wenye thamani ya Sh. milioni 150.

Alimweleza Mkuu wa mkoa kwamba mkataba wa tatu ambao wamesaini ni wa kuleta mita za malipo ya kabla-ambao mamlaka hiyo inatarajia kupata dira za malipo ya kabla 300 kutoka moja ya Kampuni ya China-mkataba ambao una thamani ya Sh. milioni 142.

“Mkataba wa nne ambao tumesaini ni wa kuleta vifaa vya maunganisho ya bomba pamoja na bomba za chuma kwa ajili ya maunganisho mapya kwa wateja wapatao 1500-ambapo kati ya hao wateja 1000 wataunganishwa kwa miji ya Manyoni na Itigi na wateja 500 itakuwa ni kwa maeneo ya Singida Mjini pamoja na sehemu ya mji wa Kiomboi huku mikataba yote hiyo ikitarajiwa kukamilika mapema 2022,” alisema Nzamba.

Awali, Dk. Mahenge pamoja na kumpongeza Rais Samia kwa juhudi za utekelezaji wa miradi hiyo muhimu kwa jamii ikiwamo huduma hiyo ya maji, aliwataka wazabuni waliokabidhiwa dhamana ya kujenga miradi hiyo kuhakikisha wanazingatia ubora na viwango.

“Kajengeni miradi imara, yenye ubora, yenye viwango lakini mkajenge kwa wakati unaotakiwa ili wananchi waweze kupata huduma hii muhimu ya maji,” alisema Mahenge na kuongeza;

“Shabaha iliyopo kwa Mkoa wa Singida ni kuhakikisha usambazaji wa huduma ya maji vijijini inakwenda kufikia zaidi ya asilimia 80 huku ile ya mijini ikifikia zaidi ya asilimia 90 muda mfupi baada ya kukamilika kwa utekelezaji wa mikataba hii.”

Mkazi wa Kijiji cha Mwankoko, Neema Khambi, aliishukuru serikali inavyopambana kusogeza huduma hiyo muhimu kwa jamii ikizingatiwa maji ni kila kitu kwa ustawi wa afya, elimu na maendeleo

## Akagua ujenzi madarasa Sikukuu Krismasi

**Na Steven William,** IRINGA

MKUU wa Wilaya ya Iringa mjini, Mohamed Moyo amelazimika kukagua na kusimamia ujenzi wa madarasa ya sekondari Sikukuu ya Krismasi, kuhakikisha yanakamilika kwa wakati.

Moyo alikuwa katika ziara hiyo juzi kuangalia shughuli za ujenzi wa madarasa hayo yanayojengwa kwa fedha za UVIKO-19.

Akieleza sababu ya kufanya ziara hiyo wakati wa sikukuu, alisema hawezi kuwa na amani wakati madarasa yakiwa hayajakamilika na kulazimika ahamishie ofisi yake katika eneo la ujenzi.

Moyo alisema kuwa mafundi wa ujenzi huo wa madarasa, kamati ya ulinzi na usalama na watendaji wa serikali na kamati za ujenzi wote walikuwa katika eneo hilo la ujenzi huo.

Alisema walikuwa chakula cha sikukuu eneo la ujenzi na kuahidi hata mwaka mpya atafanya hivyo lengo likiwa kukamilisha madarasa hayo kwa wakati na kukabidhiwa.

Moyo alisema Wilaya ya Iringa mjini ipo mbioni kukamilisha ujenzi huo katika shule za sekondari 66 zikiwamo shule shikizi 28 ili wanafunzi wanaoanza kidato cha kwanza mwakani waingie katika madarasa.

Alisema baadhi ya shule ujenzi wa madarasa umefikia hatua za mwisho kwa kuweka madirisha ya vioo.

Kadhalika alisema wakati wowote kuanzia sasa mafundi watakabidhi vyumba hivyo kwa kuwa ujenzi umefikia hatua za mwisho.

Moyo alikagua ujenzi wa vyumba vya madarasa katika shule za sekondari za Nyerere, Nyang’oro, Furahia, Kiwale, Ilambilole, Isimani na za shikizi ambazo ni Kibaoni, Kigasi, Ikengeze zilizo katia hatua ya umaliziaji ujenzi wake kwa kuwekwa marumaru.

**Moyo alisema kuwa mafundi wa ujenzi huo wa madarasa, kamati ya ulinzi na usalama na watendaji wa serikali na kamati za ujenzi wote walikuwa katika eneo hilo la ujenzi huo.**

# Muda wa usalimishaji silaha waongezwa

**Na Elizabeth Zaya**

WAZIRI wa Mambo ya Ndani, George Simbachawene ametoa nafasi nyingine kwa wanaomiliki silaha kinyume cha sheria kuzisalimisha kabla ya msako na hatua kali kuchukuliwa dhidi yao.

Akizungumza na waandishi wa habari jana jijini Dar es Salaam, alisema msako wa silaha hizo ni endelevu na kwamba watakaokutwa nazo nyumbani bila kuziwasilisha kwa hiari yao watachukuliwa hatua kali za kisheria.

"Uwasilishaji wa silaha kwa hiari uliotangazwa na Rais Samia Suluhu Hassan umekwenda vizuri sana na tulitoa taarifa kwamba tumepata mafanikio makubwa, lakini tunaamini kwamba zipo silaha nyingine ambazo zinamilikiwa na baadhi ya wananchi kinyume cha sheria," alisema na kuongeza;

"Bado tunatoa rai kwamba ukijisikia unaweza kurudisha, lakini kama katika misako yetu ambayo imeanza sasa na itakuwa endelevu, ukikamatwa utaingia kwenye matatizo makubwa sana."

"Ni vyema badala ya watu kukamatwa kupitia misako hiyo kutumia uhuru ambao ulitolewa na Rais, kwamba wanaomiliki silaha kinyume cha sheria wazirejeshe na hata sasa mtu ukijisikia una silaha ambayo unaimiliki na huelewi mazingira ya utaratibu ulivyoipata, ukirejesha unaweza kuwa uko salama zaidi kuliko ukiendelea kuitumia halafu ukaja kukamatwa kwako kwa msako unaoendelea."

VITAMBULISHO VYA TAIFA

Kuhusu utoaji wa Vitambulisho vya Taifa, Simbachawene alisema wako katika hatua za mwisho za kuanza kutengeneza kwa awamu ya pili.

Alisema katika awamu hiyo wanatarajia kuvitengeneza kwa wingi na kwa kasi kubwa tofauti na ilivyokuwa awali.

"Vitambulisho vya Taifa tulishasema mara nyingi, kwa sasa tuko katika hatua za mwisho za kutengeneza kwa awamu ya pili ambayo sasa vitakuwa vinazalishwa kwa wingi sana na tutapata vitambulisho kwa kasi kubwa," alisema Simbachawene.

"Na kwa sasa karibu kila mkoa kuna vitambulisho ambavyo wanaotakiwa kuvichukua hawajavichukua, karibu kila mkoa, kila wilaya, watu wametengenezewa lakini hawafiki kwenda kuvichukua. Kwa hiyo tusipeleke tu lawama kwa Mamaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA) pekee, lakini pia hata walioagiza wengine vitambulisho hivyo hawajafika kwenda kuvichukua na ni vizuri wananchi tukawa tunafuatilia kule ambako tulikoombea. Wengine ambao bado hawajapata, tunaendelea na mchakato wa kuvitengeneza."

# Ofisa mifugo afariki usingizini

**Na Samson Chacha,** TARIME

OFISA Mifugo wa Halmashauri ya Mji Tarime, Pedas Masungwa, aliyetarajiwa kustaafu mwakani, amefariki dunia akiwa usingizini.

Mkurugenzi Mtendaji wa halmashauri hiyo, Gimbana Ntovya, alithibitisha kutokea kwa kifo hicho kilichotokea Desemba 27, mwaka huu.

"Halmashauri yetu tumepata pigo kwa kumpoteza mtumishi mwenzetu Pedas usiku wa kuamkia Jumatatu, na taarifa za madaktari zinaeleza kuwa kifo chake kilitokana na shinikizo la damu (BP)," alisema.

Kwa mujibu wa Ntovya, familia yake ilisema Pedas alifika nyumbani kwake usiku na kwenda kulala, lakini baadaye alisikika akikoroma kwa sauti hali iliyomfanya mke wake na watoto kwenda kumwamsha bila mafanikio.

Alisema familia hiyo ilibidi iombe msaada kwa majirani kumpeleka hospitali, lakini alikuwa ameshapoteza maisha.

Kwa mujibu wa Mkurugenzi huyo, mwili wa marehemu unatarajiwa kuzikwa kijijini kwake Musoma, mkoani Mara.

"Masungwa alikuwa mzalendo alijituma kwa kazi yake ya kuhudumia mifugo hata katika minada aliwahudumia wananchi, wafugaji kwa kutoa elimu kwa vitendo," alisema.



Mwenyekiti wa Bodi ya Nishati Vijijini (REB) Wakili Julius Kalolo (wa pili-kushoto) na Mkurugenzi Mkuu wa Wakala wa Nishati Vijijini (REA) Mhandisi Hassan Saidy (kulia) wakijadiliana jambo wakati walipokuwa katika ziara ya kazi wilayani Kibondo kukagua utekelezaji wa miradi ya umeme mwishoni mwa wiki. PICHA: MPIGAPICHA WETU

# Wafukua kaburi na kuvunja jeneza

**Na Neema Hussein,** KATAVI

KABURI la marehemu Veronika Wambali (63), aliyezikwa juzi saa tisa alasiri katika makaburi ya Mwangaza, Manispaa ya Mpanda, mkoani Katavi, limefukuliwa na watu wasiojulikana kisha jeneza lake kuvunjwa na kuachwa wazi.

Akizungumza na Nipashe, Mwenyekiti wa Mtaa wa Mpadeco, Kata ya Makanyagio, Ivo Chambala, alisema tukio hilo limetokea jana baada ya kupokea taarifa kutoka kwa wapita njia.

Chambala alisema ndugu wa marehemu walipofika eneo alilozikwa ndugu yao, walishirikiana kutoa taarifa polisi na kuthibitisha kuwa jeneza lilivunjwa na mwili kuachwa.

"Jana nimeshiriki kumzika marehemu, ndugu zake nilikuwa nawafahamu cha ajabu leo (jana) kaburi limefukuliwa sasa ndiyo tumerudi tena kuzika upya na kulifanyia marekebisho kaburi," alisema.

Kwa upande wake, msemaji wa familia, Chifu Mulela Mallac, alisema Veronika alifariki Desemba 23 na mwili wake kusafirishwa mkoani Katavi kwa ajili ya mazishi na waliupokea mwili huo Desemba 25 na kuuzika siku iliyofuata.

Alisema wameshangazwa na kitendo cha kufukuliwa kaburi na kuvunjwa kwa jeneza, huku mwili ukiachwa.

Alisema tukio hilo limewaacha na maswali mengi bila majibu sahihi kwamba waliotenda walitaka nini.

"Sisi kama familia tumejiuliza mambo mengi sana waliofanya uovu huu walikua wanataka nini marehemu alikuwa ni mtu wa kawaida hakuwa na uwezo wowote na alikuwa ni mtu mzima tu maana alizaliwa mwaka 1958 hivyo alikua na miaka 63, sasa sijui shida yao hasa ilikuwa ni nini," alihoji Mallac.

Baadhi ya wananchi walioshuhudia tukio hilo, akiwano Mikidadi Idd, walisema wamesikitishwa na tukio hilo ambalo walilihusisha na imani za kishirikina.

## MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Kilio cha Katiba mpya kisikilizwe

**KIU** ya kupatikana kwa Katiba mpya inazidi kuongezeka huku mjadala ukiendelea kwenye mitandao ya kijamii kwa wanasiasa na wananchi kuona umuhimu wake.

Kwa sasa kila linapotokea jambo la kitaifa linalosababisha utengano wengi huelekeza kilio kwenye Katiba mpya, huku wakigusia Tume Huru ya Uchaguzi, mamlaka ya Rais kuteua, kuruhusu kupinga matokeo ya urais mahakamani, mgombea binafsi na upatikanaji wa mawaziri.

Mjadala ulishika kasi zaidi wakati wa mkutano wa Baraza la Vyama vya Siasa, ambalo lilitoka na maazimio 80 moja wapo likiwa ni umuhimu wa Katiba mpya.

Pia, wadau kama Mtandao wa Madeni na Maendeleo Tanzania (TCDD), nao wameanza mchakato wa kukusanya saini 5,000 za Watanzania wa makundi mbalimbali, ili wawasilishe kwa Rais Samia Suluhu Hassan kuonyesha umuhimu wa kuanza kwa mchakato huo.

Baadhi ya viongozi wa vyama vya siasa nao wamejitokeza mbele ya vyombo vya habari na kwenye mitandao ya kijamii kueleza umuhimu wa kuweka 'viraka' kwenye Katiba ya mwaka 1977 kufanya marekebisho ya muundo na namna wateule wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) wanavyopatikana.

Kwa muda mrefu kumekuwa na malalamiko kuwa NEC haiko huru kwa kuwa Makamishna wake wanateuliwa na Rais ambaye ni Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi ambacho kinashiriki uchaguzi kushindania kiti cha urais, ubunge na udiwani kama vyama vingine.

Pia, uchaguzi husimamiwa na Wakurugenzi Watendaji wa Halmashauri ngazi ya majimbo, ambao ni wateule wa Rais.

Mchakato wa Katiba mpya ulianzishwa na Rais Jakaya Kikwete kwa kuunda Tume ya Marekebisho ya Katiba chini ya uenyekiti wa Jaji Joseph Warioba, ambayo iliwasilishwa kwenye Bunge Maalumu la Katiba, lakini mchakato ulifika mwisho wajumbe wakiwa wamegawanyika.

Kwa sasa kumekuwa na mtanziko wa wapi pa kuanzia kwa kuwa wapo wanaoikubali Katiba pendekezwa na wanadai ni kama Katiba ya sasa imewekewa 'viraka' na wengine wakisema haikuhusisha wote kwa kuwa wajumbe wa vyama vya upinzani walisusia bunge hilo na kuunda Umoja wa Katiba ya Wananchi (UKAWA) huku wajumbe wa CCM na makundi mengine wakibaki hadi mwisho na kutoa Katiba pendekezwa.

Kwa mujibu wa Sheria ya Mabadiliko ya Katiba wakati ule ilipaswa kuwa na makundi mawili yanayounga mkono na yanayopinga kufanya kampeni kabla ya kuwa na kura ya maoni ambayo ingepigwa na Watanzania wote kuamua iwe Katiba.

Kutokana na mkwamo huo bado maswali ni mengi kama maoni ya wananchi yatakusanywa tena, kwenye rasimu ya Jaji Warioba au Katiba Pendekezwa? Na ndiyo maana hadi imeendelea kutumia iliyopo.

Juzi Mwenyekiti wa CUF Taifa, Prof. Ibrahim Lipumba, alipendekeza kufanyika marekebisho ya Katiba kwa kuweka Tume Huru ya Uchaguzi na ipatikane kabla ya uchaguzi mkuu wa 2025, kwa kuwa ili kuwa na Katiba mpya inahitaji miaka mitatu kabla ya kuanza kutumika.

Rais Samia alisema apewe muda aimarishe maendeleo ya uchumi wa nchi kwanza kisha suala la Katiba litajadiliwa, lakini wapo wanaosema maendeleo yanakwenda pamoja na Katiba ambayo ni sheria mama.

Kuna umuhimu wa ya kilio hiki kusikika hasa kwa ibara muhimu ambazo zinaonekana zinahitaji kufanyiwa marekebisho na hata viongozi wa vyama vya siasa waliokutana Dodoma waliona umuhimu wake.

Katiba iliyopo sasa ilitungwa wakati nchi haijawa na watu wengi wala mahitaji hayakuwa kama ya sasa na ndiyo maana msukumo umekuwa mkubwa kwa kuwa sasa nchi ina vyama vingi hivyo ni muhimu jambo hili likapewa kipaumbele ili kupunguza au kuondoa malalamiko kwenye uchaguzi mkuu ujao.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:

**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lymo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Watoto ombaomba kuzurura bila kusoma ni kuandaa bomu kesho

Na Sabato Kasika

**TANZANIA** inafanya harakati mbalimbali za kuwakwamua watoto na ujinga kwa kutoa elimu kwa wote, kwa kuzingatia kwamba, elimu ya msingi kwa kila mtoto ni lengo namba mbili la Maendeleo Endelevu ya Milenia (MDGs).

Lengo hilo linasisitiza kuhusu umuhimu wa kuwa na elimu kwa wote ili kuwezesha maendeleo katika sekta zote na Tanzania inajitahidi kulitimiza lengo hilo siyo tu kwenye ujenzi wa madarasa, bali pia kwa kuongeza kiwango cha uandikishaji wa watoto wa elimu ya awali na darasa la kwanza ili wapate elimu hatimaye wasonge mbele zaidi kulingana na uwezo wa kitaaluma darasani.

Hata hivyo, pamoja na juhudi hizo, bado wapo baadhi ya watu ambao kutokana na sababu mbalimbali zikiwamo umaskini hawasomi ama wazazi hawawapeleki watoto wao shuleni. Kwa mfano mmojawapo ni watoto ambao kila siku husimama katika barabara mbalimbali za jijini Dar es Salaam wakiomba pesa kutoka kwa abiria au kwa madereva wa magari yanayopita mbele yao.

Wengi wao walitakiwa kuwa darasani lakini wakati wa masomo, wako barabarani wakiomba msaada wa fedha na wengine wakisafisha vioo vya magari ili wapate ujira, na wakati mwingine wanafungiwa vioo na kufukuzwa kwa kuchafua magari ya watu.

Ni wazi kwamba, kuna haja ya kuchukua hatua za makusudi kusaidia kundi hilo ambalo ni miongoni mwa wale wanaotarajiwa wa taifa la kesho, kama ilivyofanyika kwa wafanyabiashara wa machinga.

Wapo vijana wadogo ambao hufanya kazi ya kusafisha magari ambao wanadai kulipwa fedha hata kama hawajaruhusiwa kusafisha vioo hivyo, haina maana kuendelea kuwa na watoto wanaoishi mitaani, serikali ichukue hatua.

Hawa ni watoto wanaohitaji kulindwa , kutunzwa na kuendelezwa kila idara na kubwa zaidi wakiheshimiwa utu wao bila kukutana na vikwazo , lakini wanalazimisha kusafisha vioo vya magari bila kuruhusiwa, kisha wanalazimisha kulipwa ujira, na kama hawakulipwa, inaelezwa kuwa wakati mwingine huwamwagia madereva maji.

Vijana hao na wengine wanaoomba pesa, hupenda kuwa maeneo yenye taa za kuongoza magari, na pale yanaposimama ili kusubiri taa ziruhusu, wao ndipo hufanya kazi hiyo iwe ni kusafisha vioo au kuomba fedha. Kwanini watoto waishi barabarani? Mkuu wa Mkoa, Idara ya Ustawi na Maendeleo ya Jamii, polisi na wadau wengine wana jukumu la kuokoa watoto hawa ambao ni jukumu la serikali kuwalinda na kuwatunza.

Wakazi wa Dar es Salaam ni mashuhuda wa hali hiyo ambayo ni vyema sasa hatua zaidi zikachukuliwa ili kuwasaidia watoto hao kupata elimu, wakati huu serikali inapogharamia elimu na kwamba bila kuwapo kwa hatua za kuhakikisha watoto hao wanakwenda shule, inawezakana wakawa bomu la baadaye.

Na hasa wale wanaosafisha vioo vya magari, kisha wanaotumia nguvu kutaka pesa kutoka kwa madereva, huenda baada ya hapo hujiingiza kwenye uhalifu kama dawa za kulevya, udokozi, unyanyasaji wenzao na hata kuharibu mali za watu mitaani.

Tutafakari kwamba, bado ni watoto, lakini wanatumia nguvu kutaka pesa. Je, wakiwa watu wazima itakuaje? Ni vyema ikawekwa mikakati ya kuhakikisha wanapelekwa shule ili wapate elimu.

Inawezekana katika kundi hilo kukawa na viongozi, wataalamu wa fani mbalimbali wa taifa la kesho, lakini hawajapata fursa ya kusoma kutokana na sababu zilizo nje ya uwezo wao au ndani ya uwezo wao.

Wakuu mbalimbali ambao wamewahi kuongoza mkoa wa Dar es Salaam kwa nyakati tofauti, walikuwa na mipango ya kuwaondoa ombaomba mitaani, lakini hata hivyo haijawahi kufanikiwa ni wakati wa kutumia mikakati mipya na bora zaidi.

HABARI KITAIFA

# Wafungwa 5,704 wasamehewa

Na Elizabeth Zaya

RAIS Samia Suluhu Hassan ametoa msamaha kwa wafungwa 5,704 katika kuadhimisha miaka 60 ya Uhuru wa Tanzania Bara.

Akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana, Waziri wa Mambo ya Ndani, George Simbachawene, alisema Rais Samia ametoa msamaha huo chini ya ibara ya 45(1) (d) cha Katiba.

Kwa mujibu wa Simbachawene, Rais Samia ametoa msamaha kwa wafungwa hao kwa masharti ya kupunguziwa robo ya adhabu zao baada ya punguzo la kawaida la moja ya tatu inayotolewa chini ya kifungu cha 49(1) cha Sheria ya Magereza, sura ya 58.

Alisema msamaha huo utawahusu pia wafungwa wenye magonjwa ya kudumu, wazee, wenye umri wa miaka 70 na zaidi, wenye ulemavu wa mwili na akili.

Wengine ni walioingia gerezani wakiwa na mimba, wanaonyonyesha na wasionyonya, pamoja na wafungwa waliokaa gerezani kwa muda wa miaka 20 na kuendelea wenye tabia njema, waliohukumiwa adhabu ya kuwekwa kizuizini ambao wamekaa gerezani kuanzia miaka 15 kuendelea.

Simbachawene alisema wafungwa ambao hawatahusika na msamaha huo ni wale wanaotumikia adhabu ya kunyongwa na wenye makosa ya kujaribu kuuwa, kujiua au kuua watoto wachanga.

Wengine ni wanaotumikia kifungo chini ya sheria ya Parole, sheria ya huduma kwa jamii na kifungo cha nje, waliopatikana na hatia ya kuhukumiwa kifungo kwa makosa ya sheria ya uhujumu uchumi, wanaotumikia vifungo kwa makosa ya matumizi mabaya ya madaraka, utakatishaji fedha, rushwa, na usafirishaji dawa za kulevya.

Wengine ambao hawatahusika na msamaha huo ni waliopatikana na hatia na kuhukumiwa kifungo kwa kosa la utekaji au wizi wa watoto, kufanya biashara ya binadamu, kuwapa mimba wanafunzi, ukatili dhidi ya watoto na wenye makosa ya kukutwa na viungo vya binadamu.

Wengine ni wenye kujihusisha na nyara za serikali, ujangili, wizi na ubadhilifu wa fedha za serikali, wafungwa wanaotumikia vifungo kwa makosa ya kutoroka au kujaribu kutoroka chini ya ulinzi halali au kusaidia kutenda makosa hayo.

**WANAORUDIA MAKOSA**

Simbachawene alisema serikali inaweka utaratibu wa kufuatilia mienendo ya wafungwa watakaosamehewa na kwamba endapo itabainika wamerudia tena kujihusisha na makosa ya jinai, watarudishwa gerezani.

"Hatuwezi kuacha kumuachia mfungwa kama ameonyesha tabia njema, isipokuwa tunaweka utaratibu mzuri wa kufuatilia mienendo ya wanaojihusisha tena na makosa ya jinai ili kabla hawajatenda tena makosa zaidi tuwarudishe gerezani,"alifafanua Waziri Simbachawene.

## Watakiwa kujikinga UVIKO-19 kwa kupata chanjo

Na Mwandishi Wetu, PEMBA

WANANCHI wa Wilaya ya Mkoani, kisiwani hapa wamewashauriwa kufuata maelekezo ya wataalamu wa afya kwa kuendelea kuvaa barakoa, kunawa mikono na kupata chanjo ya UVIKO-19 ili kulinda usalama wa afya zao.

Akizungumza na mwandishi wa habari hizi, Mkurugenzi wa Baraza la Mji Mkoani, Yussuf Kaiza Makame, alisema licha ya wananchi kuchukua tahadhari za kujilinda ni vyema wakafuata maagizo wanayopatiwa na wataalamu wa afya.

Alisema, baadhi ya watu wanapuuza agizo la wataalamu wa afya jambo linaloweza kusababisha maambukizi ya ugonjwa huo kusambaa zaidi.

"Tunajikinga ila ni kwa kiasi kidogo sana kwa sababu tunaona kama ugonjwa haupo tena, tusijisahau wananchi, tuendelee kujikinga na kuwakinga wengine," alisema.

Ofisa Afya Baraza la Mji Mkoani, Bimkubwa Kheir alisema, kila mwananchi anatakiwa ajitambue kuwa ni muathirika wa ugonjwa huo, kwa kuwa athari zitakazotokea zinampata kila mmoja kwa namna moja ama nyingine.

"Tuliopata chanjo tujitahidi kuwahamasisha wengine na wao wachome, kujikinga ni bora zaidi, tusikae mitaani na kuzungumza dhana potofu kuhusu chanjo," ni salama na haina madhara," alifafanua ofisa huyo.

Naye Mratibu wa Elimu ya Afya Pemba, Abeid Ali, alieleza muhimu wa chanjo kuwa unazuia maambukizi ya ugonjwa wa corona kwa asilimia kubwa.



Naibu Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu Kazi, Vijana na Ajira, Patrobas Katambi, ambaye pia ni Mbunge wa Jimbo la Shinyanga Mjini, akikagua ubora wa Ubao katika shule ya sekondari Kolandoto Manispaa ya Shinyanga, leo/ jana, alipofika kukagua maendeleo ya ujenzi wa vyumba viwili vya madarasa shuleni hapo, kwa fedha za UVIKO 19 Sh.milioni 40 na kuridhishwa na hatua ya ujenzi wa vyumba hivyo. PICHA: MARCO MADUHU

## Rais ateua Mwenyekiti NEC, Bodi ya Mikopo

Na Mwandishi Wetu

RAIS Samia Suluhu Hassan amemteua Jaji Jacob Mwambegele, kuwa Mwenyekiti wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC).

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa jana na Mkurugenzi wa Mawasiliano ya Rais, Ikulu, Jaffar Haniu, Mwambegele ni Jaji wa Mahakama ya Rufani na Mjumbe wa NEC, anayechukua nafasi ya Jaji mstaafu wa Mahakama ya Rufani, Semistocles Kaijage, aliyemaliza muda wake.

Pia, Rais amemteua Jaji Mwanaisha Kwariko kuwa mjumbe wa NEC akichukua nafasi iliyoachwa wazi na Jaji Mwambegele.

Mwingine aliyeteuliwa ni Jaji wa Mahakama Kuu, Sam Rumanyika kuwa Jaji wa Mahakama ya Rufani.

Katika hatua nyingine, Rais amemteua Prof. Khamis Dihenga kuwa Mwenyekiti wa Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB).

Taarifa hiyo ilibainisha kuwa kiongozi huyo anahudumu kwa mkataba katika Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine (SUA), Morogoro, na anachukua nafasi ya Prof. William Anangisye, aliyemaliza muda wake.

Aliyeteuliwa mwingine ni Mhadhiri Mwandamizi wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM), Dk. Mussa Kissaka kuwa Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi wa Mamlaka ya Serikali Mtandao (eGA).

Kwa mujibu wa taarifa hiyo uteuzi huo ulianza Desemba 23, mwaka huu.

# Viongozi wa dini wakemea dhambi Sikukuu

**Na Renatus Masuguliko,**
GEITA

VIONGOZI wa dini mkoani Geita wamekemea wanaotenda dhambi wakati wa Sikukuu ya Krismasi badala ya kumrudia Mungu kwa kutenda mema.

Hayo yalisemwa hivi karibuni na baadhi ya viongozi wa Umoja wa Makanisa ya Kipentekoste mkoani humo, wakati akitoa tamko rasmi la kufanyika kwa ibada na kongamano maalumu kwa ajili ya kujitathimini na kuliombea taifa na viongozi wake kuliepusha na majanga kwa mwaka 2022 baada ya ibada ya Krismasi.

Baadhi ya viongozi hao, Katibu wa Umoja huo, Mchungaji Joshua William alisema ibada hiyo inalenga kujitathimini uwajibikaji na ushiriki katika kutimiza wajibu wa viongozi wa dini na waumini.

Viongozi wengine ni Askofu James Majembemakali, Askofu Nestory Lunyilija, Askofu Stephano Kamhanda na Dk. Robert Ngai.

Mratibu wa kongamano hilo, Mchungaji Raphael Mgalatia, alisema litafanyika Desemba 30, mwaka huu, katika uwanja wa CCM Kalangalala Geita mjini na kuwa litawashirkisha wananchi wote bila kujali dini zao kwa ajili ya kufanya tathimini kubaini changamoto za mwaka 2021 kwa kuweka mikakati ili zisijirudie 2022.

Aidha, alisema mgeni rasmi atakuwa Mkuu wa Mkoa wa Geita, Rosemary Senyamule na litakwenda sambamba na ibada maalumu kuliombea taifa, viongozi na wananchi ili Mungu awaepushe na janga la UVIKO-19.



Muuguzi katika hospitali ya halmashauri ya mji Masasi mkoani Mtwara akiendelea kumtunza mtoto kichanga ambaye wiki iliyopita aliokotwa akiwa ametupwa jalalani katika kijiji cha Chikukwe, mtaa wa Mwambao kata ya Chikukwe wilayani Masasi, kichanga hicho bado kipo katika hospitali hiyo na bado kinaendelea kuwa na afya nzuri kama kilivyotembelewa na gazeti hili jana. PICHA: HAMISI NASRI

# Katambi afurahia ujenzi wa madarasa

**Na Marco Maduhu,**
SHINYANGA

NAIBU Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana na Ajira, Patrobas Katambi, amesema ameona thamani ya fedha kwenye ujenzi wa vyumba vya madarasa katika shule za sekondari na shikizi, Manispaa ya Shinyanga.

Katambi ambaye pia ni Mbuge wa Jimbo la Shinyanga Mjini, alibainisha hayo jana kwenye ziara yake ya kukagua ujenzi wa vyumba vya madarasa, pamoja na miundombinu ya barabara na madaraja.

Alisema baada ya kukagua ujenzi huo shule za sekondari Kolandoto na Uzogole pamoja na shule ya msingi shikizi ya Zaire ameridhishwa kwa kuwa fedha imetumika ipasavyo.

"Nimekagua ujenzi wa vyumba vya madarasa kwa kweli nimeona thamani ya fedha, mmejenga kwa ubora unaotakiwa licha ya kujenga vyumba viwili vya madarasa kwa Sh. milioni 40, lakini mmejiongeza na kujenga ofisi moja ya walimu," alibainisha Katambi.

Aliwapongeza pia wananchi kwa kumuunga mkono Rais Samia Suluhu Hassan kwenye ujenzi wa vyumba hivyo kwa kutoa nguvu kazi ikiwamo kushiriki kwenye shughuli za uchimbaji msingi.

Katika hatua nyingine, akikagua ujenzi wa miundombinu ya barabara na madaraja, aliwataka Wakala wa Barabara Mjini na Vijijini (TARURA), kuongeza kasi ya ujenzi wa miundombinu hiyo, pamoja na kuzingatia ubora unaotakiwa na kuikamilisha kwa wakati.

Nao, Wakuu wa shule, Deus Maganga wa Kolandoto na Cosmas Nkoko wa Uzogole, kwa nyakati tofauti walisema ujenzi wa vyumba hivyo utasaidia kupunguza changamoto ya msongamano wa wanafunzi madarasani.

## CCM yahamasisha usajili kidijitali

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

CHAMA Cha Mapinduzi (CCM) Kibaha Mjini, kimetoa wito kwa wanachama wake kujisajili kwa njia ya kidijitali ili waingie kwenye mfumo wa kisasa.

Akizungumza juzi na viongozi wa Jumuiya ya Wazazi wa wilaya ya Kibaha, Katibu wa CCM, Ally Suleiman, alisema chama kinaingia kwenye mifumo ya kisasa na kwamba ni muhimu kila mmoja akajisajili kwa njia hiyo.

Alisema wanachama wote wanatakiwa kusajiliwa kwenye mfumo wa kielektroniki na kupata kadi za kidigitali na ifikapo 2022 wanachama wote wanatakiwa wawe wamesajiliwa kwenye mfumo huo utakaosaidia upatikanaji wa taarifa.

Alisema vipo vikwazo vya simu za kusajilia wanachama na suala hilo linafanyiwa marekebisho, ambapo vitasambazwa kila kata ili kusajili wanachama kwa njia ya kielektroniki.

Kwa upande wake, Mwenyekiti wa Jumuiya ya Wazazi Kibaha Mjini, Nuru Magege, alisema wameweka utaratibu mzuri wa kuhamasisha wanachama kujisajili.

Aidha, alisema baadhi ya viongozi walipata mafunzo ya namna ya kusajili wanachama na zoezi hilo litakwenda vizuri na kufikia malengo waliyojiwekea.

Naye Mwenyekiti wa CCM Kibaha Mjini, Maulid Bundala, alisema wanachama wanapaswa kujisajili kwa njia hiyo ambayo itasaidia kujua idadi kamili ya wanachama.

**Alisema wanachama wote wanatakiwa kusajiliwa kwenye mfumo wa kielektroniki na kupata kadi za kidigitali na ifikapo 2022 wanachama wote wanatakiwa wawe wamesajiliwa kwenye mfumo huo utakaosaidia upatikanaji wa taarifa.**

# Biteko awajia juu wanaotapeli wafanyabiashara madini wa nje

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

WAZIRI wa Madini, Dk. Doto Biteko ameonya kundi la baadhi ya wafanyabiashara wa madini ya dhahabu wanaojihusisha na vitendo vya kutapeli wafanyabishara kutoka nchi za nje kwa kuwaomba fedha ili wawanunulie madini.

Alisema matapeli hushindwa kufanya hivyo na kujificha kwenye kisingizio kuwa wanaumwa UVIKO-19.

Ameonya kuwa wizara haitavumilia vitendo hivyo kwa sababu vinadhalilisha nchi kupitia sekta hiyo na sasa wanajipanga kuanza kuwachukulia hatua za kisheria wote wanaojihusisha na vitendo hivyo.

Pia, amewatadharisha maofisa madini wanaoshirikiana na baadhi ya wafanyabiashara kuwaibia wachimbaji wadogo wa madini kwa kupaka mafuta mashine ya kupima dhahabu na kusababisha kupata kilo chache kulinganisha na madini yaliyofikishwa.

Dk. Biteko aliyabainisha hayo juzi wakati wa kikao cha wadau na wafanyabiashara wa madini kutoka mikoa 10 ya kimadini nchini, uliofanyika Halmashauri ya Manispaa ya Kahama, mkoani Shinyanga, lengo likiwa ni kusikiliza kero mbalimbali zinazowakabili wafanyabiashara hao.

Alisema kuwa, kundi hilo limekuwa likipokea fedha za ununuzi wa madini kutoka kwa wafanyabishara wa nje (wazungu) na kupiga picha maboksi ya madini yaliyofungwa siri za wizara ya madini feki kisha kuwatumia kwa njia ya WhatsApp kuwa mzigo uko njiani, jambo ambalo sio kweli na wanapotumiwa fedha wanazima simu zao.

"Hivi karibu amekuja mzungu ofisini analia kutapeliwa Dola za Kimarekani 800,000 sawa na kiasi cha Sh. bilioni 7.2, tulipompigia simu mhusika aliyepatiwa fedha hizo alirusha maneno na kusingizia kuwa anaumwa UVIKO-19 jambo ambalo sio kweli," alisema Dk. Biteko.

Aidha, alisema hapo awali wafanyabiashara wa madini walikuwa wakituhumiwa katika shughuli ya utoroshaji wa madini na kusababisha serikali kukosa maduhuri, lakini baada ya kulidhibiti jambo hilo kwa sasa wameibuka kuwatapeli wafanyabiashara wa nje fedha za ununuzi wa madini.

Hata hivyo Dk. Biteko alisema, kuna masoko ya madini yamekuwa yakifanya vyema kulipa maduhuri ya serikali bila kusumbuana na kwamba soko la madini mkoa wa Geita linaongoza nchi nzima kwa kulipa fedha hizo kwa zaidi ya Sh. bilioni 211.5 kwa kipindi cha mwaka jana.

Kadhalika, alisema soko la pili ni Mara lilipata maduhuri hayo Sh. bilioni 109.3 ikifuatiwa na soko la madini mkoa wa kimadini Kahama kwa kiasi cha Sh. bilioni 93.7 na mwaka huu wa fedha zinatakiwa kukusanywa Sh. bilioni 650.

Naye Mwenyekiti wa soko la madini Mbogwe mkoani Geita alisema, soko halina Ofisa wa Usalama wa Taifa ambaye atasimamia shughuli ya ufungaji hali ambayo imekuwa ikisababisha kuchukua muda wa usafirishaji.

Pia, Edson Charles alisema, kuna baadhi ya maofisa madini katika maeneo yao wasipowapatia posho wanashindwa kuja kuhakiki wakati wa ufungaji mzigo wa dhahabu na wamekuwa wakichelewesha kutoa namba za malipo kwa ajili ya kulipa fedha za maduhuri ya serikali..

## Aliyepinga kifungo cha miaka 30 agonga mwamba

**Na Kulwa Mzee**

MAHAKAMA ya Rufani Tanzania imetupilia mbali rufani iliyokatwa na Christian Ugbechi akipinga kifungo cha miaka 30 jela kwa kukutwa na dawa za kulevya na kubariki atumikie adhabu hiyo.

Hukumu hiyo ilitolewa na jopo la majaji watatu, Jaji Mkuye Mwambegele, Jaji Mary Levira na Jaji Issa Maige baada ya kupitia sababu 19 za kupinga hukumu iliyoletwa na Mahakama Kuu, Divisheni ya Makosa ya Rushwa na Uhujumu Uchumi.

Katika kesi dhidi ya Jamhuri, mlalamikaji alihukumiwa Juni 21, mwaka 2019 na kupewa adhabu ya kutumikia kifungo cha miaka 30 jela.

Inadaiwa alikamatwa Uwanja Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere akiwa anasafirisha dawa za kulevya gramu 947.57 aina ya heroine.

Pia, katika hati ya mashtaka mlalamikaji alikuwa akisafirisha dawa hizo kuelekea Vienna kupitia Addis Ababa, lakini hakufanikiwa kutekeleza azma yake baada ya kushukiwa na kukamatwa.

Koplo Peter na wenzake wawili walimkamata na alipopekuliwa katika begi lake alikutwa na dawa za kulevya akiwa kazihifadhi katika soksi nyeusi.

Upande wa Jamhuri uliwakilishwa na wakili wa serikali Apimaki Mabrouk na mrufani alijiwakilisha mwenyewe.

Mrufani miongoni mwa sababu za kupinga adhabu ya kifungo ni kwamba upande wa Jamhuri ulishindwa kuthibitisha makosa dhidi yake bila kuacha shaka yoyote na kwamba shahidi hakujenga msingi wa vielelezo vilivyotolewa mahakamani kuonyesha vilimfikiaje.

Pia, ilidaiwa soksi inayodaiwa zilikutwa dawa za kulevya haikutolewa kama kielelezo mahakamani.

Baada ya kupitia hoja hizo zilizopingwa na Jamhuri kwa madai upande wa mashtaka walithibitisha mashtaka bila kuacha shaka, jopo lilisema kwamba kielelezo kama soksi kilitakiwa kitolewe mahakamani.

"Pamoja na sababu hizo, mahakama inaona hakuna haja ya kugusa hukumu iliyotolewa na mahakama ya chini, kesi dhidi ya mrufani ilithibitika bila kuacha shaka, rufani inatupiliwa mbali," lilisema jopo hilo na kwamba adhabu dhidi ya mrufani inaendelea.




Meneja Mauzo wa Tigo Moshi, mkoani Kilimanjaro, Silas Mkuyu (kulia), akikabidhi zawadi ya pikipiki kwa Jeremiah Shoo, mkazi wa Machame, mshindi wa pikipiki, katika promosheni inanyoendelea ya wagiftishe gift juu ya gift, mkoani humo juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Asasi yaomba fedha za UVIKO-19 zifikirie shule za wenye ulemavu

**Na Christina Haule,** MVOMERO

ASASI za kiraia zinazoshughulikia masuala ya watoto mkoani Morogoro, zimesema suala la ujenzi wa madarasa katika shule za sekondari za kata linalofanywa na serikali nchini kupitia fedha za UVIKOO-19 sio la kubezwa na lifikiriwe pia kwenye shule za msingi na shule maalumu za watoto wenye ulemavu.

Mkurugenzi wa shule maalumu ya watoto wenye ulemavu wa viungo na akili (Amani) iliyopo wilayani Mvomero, mkoani hapa, Padre Beatus Sewando alisema jana kuwa ni vyema serikali ikafikiria kujenga madarasa ya nyongeza kwenye shule maalumu za watoto wenye ulemavu ili kutimiza uhitaji na kuwafanya wakae mbalimbali na kuepuka ugonjwa wa virusi vya corona.

Alisema suala hilo linafaa kupongezwa na kwamba wanafunzi watakaa mbalimbali darasani na kuleta maana halisi ya kujikinga na janga hilo.

Alisema uwapo wa shule maalumu ya watoto wenye ulemavu wilayani Morogoro unasaidia wazazi wengi kupata pa kukimbilia kuwapeleka watoto wao kusoma kutoka maeneo mbalimbali ya mkoa huo.

Kadhalika, alisema shule maalumu ya Amani ina jumla ya wanafunzi 70 huku ikiwa na vyumba vya madarasa vitatu na upungufu kwa asilimia 40 kwa kipindi hiki cha UVIKO-19 kinachotaka wanafunzi kukaa mbalimbali darasani.

Naye mmoja wa watu wenye ulemavu, Benedict Desdery, aliishauri serikali kuongeza madarasa hayo huku ikizingatia kuboresha miundombinu kwenye shule hizo.

Alisema awali shule hizo za kata hazikuwa na miundombinu rafiki kwa ajili ya watu wenye ulemavu wa viungo jambo ambalo lilimuwia vigumu wakati akisoma sekondari na kulazimika kusukumwa na wenzie au kubebwa katika baadhi ya maeneo shuleni licha ya kuwa na baiskeli ya miguu mitatu.

Naye Mkurugenzi wa Asasi ya Wezesha Mabadiliko, Dk. Lusako Mwakiluma, aliishauri serikali kupitia fedha hizo kuongeza madarasa pia katika shule za msingi ili kuwafanya wanafunzi kuepuka msongamano mkubwa uliopo ikiwamo uwapo wa wanafunzi wanaokaa chini madarasani kwa sasa.

Serikali imetenga kiasi cha Sh. trilioni 1.3 zilizokuja kwa ajili ya UVIKO-19 kwa kuzifikisha kwenye sekta mbalimbali ikiwamo elimu na maji ili kutengeneza miundombinu na kujikinga na ugonjwa huo.

# Ndumbaro kusomesha watoto wanne sekondari

**Na Amon Mtega,** SONGEA

WAZIRI wa Maliasili na Utalii ambaye pia ni Mbunge wa Jimbo la Songea mjini mkoani Ruvuma, Dk. Damas Ndumbaro, amejitolea kuwasomesha sekondari watoto wanne wanaolelewa katika vituo vya watoto wanaoishi katika mazingira magumu ikiwa ni mchango wake kuunga mkono juhudi za serikali.

Alisema baada ya kubaini changamoto zinazowakabili watoto hao aliamua kuanzisha mchezo wa gofu ambao uliwakusanya marafiki zake wengi kisha kumchangia fedha kwa ajili ya watoto hao.

Dk. Ndumbaro alijitolea kusomesha watoto hao alipotembelea vituo vitatu vya kulelea watoto hao, vikiwamo vya Mtakatifu Anthony kilichopo kata ya Mfaranyaki, Swacco kilichopo Mwengemshindo na Mtakatifu Tereza kilichopo Msamala na kutoa zawadi za Sikukuu ya Krisimasi na kuwatakia heri ya Mwaka Mpya wa 2022.

Waziri huyo akiwa ameambatana na Meya wa Manispaa ya Songea, Michael Mbano, Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Hamis Abdallah Ally na familia yake amesema kuwa kama jamii itajenga tabia ya kuwatembelea watoto wanaolelewa kwenye vituo hivyo, matatizo yanayowakabili yatatuliwa.

Dk. Ndumbaro alitoa zawadi mbalimbali ukiwamo mchele, unga, sukari, mafuta ya kupikia vyakula na mafuta ya kupaka mwilini, sabuni pamoja na vinywaji baridi ikiwa ni sehemu ya kusherehekea Sikukuu ya Krismasi.

Alisema kuwa watoto waliyopo kwenye vituo hivyo ni wa wote, hawawajui wazazi wao zaidi ya wale wanaokwenda kuwatembelea na kuwapa misaada.

Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori (TAWA), wakiwa wameambatana na waziri huyo wamechangia magodoro huku kituo cha Swacco kikiwa kimepatiwa vitanda sita vyenye mfumo wa mbili kwa moja ili kuboresha mazingira ya kulala watoto hao.

Kwa upande wake Mwenyekiti wa CCM wilaya ya Songea Mjini, Ally aliwapongeza wanaosimamia vituo hivyo kuwa wana moyo wa upendo jambo ambalo jamii inatakiwa kujifunza.

Meya wa Manispaa ya Songea, Mbano alisema manispaa hiyo itaendelea kushirikiana na vituo vyote vya kulelea watoto kwenye manispaa hiyo ili kubaini changamoto wanazokutana nazo.

Naye mmoja wa walezi wa watoto hao mtawa Judith Mwageni wa kituo cha Mtakatifu Anthony, alisema watoto hao huchukuliwa katika mazingira hatarishi na changamoto za kuwatimizia mahitaji yao ni kubwa.

Kwa upande wao watoto hao wamemshukuru waziri huyo kwa upendo wake, huku baadhi wakitoa zawadi ya keki kwa waziri ikiwa ni sehemu ya kutambua mchango wake na kuwatembelea mara kwa mara.



Waziri wa Maliasili na Utalii ambaye pia ni Mbunge wa Jimbo la Songea mjini Dk. Damas Ndumbaro akimkabidhi zawadi mbalimbali kwenye kituo cha Mtakatifu Anthony kilichopo Mfaranyaki alipokuwa ametembelea vituo vitatu vya kulelea watoto hao. **PICHA NA AMON MTEGA.**

# Asas achangia mil. 10/- ujenzi ofisi ya CCM

**Na Francis Godwin,** IRINGA

MJUMBE wa Halmashauri Kuu ya CCM Taifa (NEC) Mkoa wa Iringa, Salim Abri Asas, amechangia Sh. milioni 10 kwa ajili ya ukamilishaji jengo la ofisi ya Chama cha Mapinduzi wilaya ya Kilolo.

Asas amekabidhi fedha hizo juzi wakati wa kikao cha Halmashauri Kuu ya CCM wilaya ya Kilolo, huku akiwataka viongozi wa wilaya hiyo kusimamia ujenzi wa ofisi hiyo ili Mei mwakani wilaya hiyo iwe imekamilisha ujenzi huo.

"Pamoja na watendaji wetu wa serikali kuendelea kutekeleza ilani, viongozi wa CCM msijifungie ndani tokeni nje nendeni mkafuatilie utekelezaji na kuwahoji pale ambapo mnaona kuna kusuasua kwa utekelezaji wa ilani ya CCM na kuna malalamiko ya wananchi," alisema Asas.

Alisema msimamizi mkuu wa ujenzi wa barabara ni TARURA au TANROADS, lakini hawajawahi kujibu maswali ya wananchi kuhusu kero ya barabara zaidi ya kuwauliza viongozi waliowachagua.

Aidha, Asas alipongeza jitihada zilizofanywa na serikali kukabiliana na tatizo la upungufu wa vyumba vya madarasa nchini.

"Hii neema ambayo imeshuka mwaka huu chini ya Rais Samia haijawahi kutokea miaka iliyopita serikali ilikuwa ikitoa agizo kuwa msipokamilisha ujenzi wa vyumba vya madarasa hadi tarehe fulani mtakiona na fedha hakuna ila sasa unaambiwa usipokamilisha ujenzi wa vyumba vya madarasa hadi Januari 15 utakiona na fedha hizi hapa kwa hiyo hakuna cha kujitetea," alisema.

Aliwataka viongozi wa CCM kwenda kuwaeleza wananchi mazuri ambayo serikali imeendelea kuyafanya na kuna mengi yanakuja kama miradi ya maji na mingine mingi ambayo serikali imeendelea kutekeleza katika maeneo mbalimbali.

Kuhusu tatizo la pembejeo za kilimo, Asas alisema ana imani serikali ipo kwenye mchakato wa kuzitatua ili kuona wakulima wanapata mbolea kwa gharama nafuu zaidi.

"Changamoto zipo, wapo ambao wameanza kulalamika hata suala la mvua kutonyesha lawama wanaitupia serikali, ndugu zangu tuwe wa kweli hili la mvua tatizo kubwa ni sisi wenyewe tunakata miti ovyo sasa kama hatutunzi mazingira tusitegemee kupata mvua za kutosha lazima tuhimizane kutunza mazingira ili kuepusha ukame," alisema.

Akizungumzia siasa, alisema mkoa wa Iringa kwenye wilaya nyingine zote hali ni nzuri na za kistaarabu zaidi, lakini kwa wilaya ya Kilolo wanachama wake ni mabingwa wa kuendesha siasa za kuchafuana na ni wilaya inayoongoza kuwa na siasa zisizofaa za kuchafua watu.

" Mimi niwaombe sana wana CCM Kilolo ni vizuri mtu kama hamtaki kutompa kura kuliko kumchafua na kura kumnyima tunatambua kuwa mwakani tunakwenda kwenye uchaguzi wa chama niwaombe tuwe na siasa za kistaarabu tuache siasa za kuchafuana," alisisitiza.

Mwenyekiti wa CCM wilaya ya Kilolo, Kilian Myenzi, aliwataka wana CCM kuendelea kushikamana kukamilisha ujenzi huo wa ofisi huku akipongeza utendaji kazi wa Rais Samia kuwa umeendelea kuwa nuru kubwa kwa chama na serikali .

# Wanaume wahusishwa tatizo udumavu kwa watoto

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

WANAUME wilayani Njombe, mkoa wa Njombe wameshauriwa kusaidia malezi ya watoto kwa kuzingatia lishe bora ili kuondokana na tatizo la udumavu.

Ushauri huo umetolewa katika mdahalo wa lishe uliofanyika mjini hapa kuwa tatizo hilo linazidi kutokana na wanaume kujiondoa katika malezi kwa kudhani ni jukumu la mama pekee na kusababisha udumavu kuzidi kuwapo.

"Suala la malezi na kuhakikisha lishe bora kwa mtoto ni la baba na mama, lakini inasikitisha kuona mama ndiyo anahangaika kuhakikisha mahitaji kwa mtoto wakati baba yupo na shughuli zake, hii si sawa," alisema Amina Said.

"Wanaume naomba twende sambamba kwenye hili ili kuhakikisha mtoto anapata afya bora, tukiungana tatizo la udumavu katika mkoa wetu litakua historia," alisema Aurelia Mtitu.

Naye Emilia Msafiri alisema kinamama wanajikita katika shughuli za kiuchumi badala ya kuweka uangalizi kwa mtoto hali inayosababisha udumavu.

"Ni kweli tunatafuta fedha, lakini tujiulize fedha hizi tunatafuta kwa ajili ya nani? Unakuta mama anaamka saa 12 asubuhi kwenda shamba nyumbani amemuachia mtoto kande tena za siku tatu huyu mtoto atakua kweli, hiyo lishe bora itatoka wapi tubadilike tuwape hawa watoto mpangilio bora wa chakula," alisema Emilia.


Kwa upande wake, Philoteus Ngilangwa, alisema wazazi wengi wanawapa watoto wao chakula ili washibe hali inayosababishwa na ukosefu wa elimu sahihi juu ya lishe.

Alisema ili kupunguza tatizo hilo elimu itolewe kuanzia ngazi za chini kama mashuleni, vyuoni na kwenye familia, wazazi/walezi wafundishwe namna ya kutumia muda vizuri wa malezi na shughuli za kuwaingizia kipato sambamba na viongozi wa umma wachukue kama ajenda katika vikao vyao.

Nipashe
# TESA
Jumanne Desemba 28, 2021
TEKNOLOJIA • ELIMU • SAYANSI


Ukurasa 12

KULENGA VITA UVIKO 2021
2022 ulete kasi, ari ,nguvu mpya viongozi, jamii waache mazoea


Ukurasa 13

Wasomi walioibuka na kinasa sumu ya nyuki


Ukurasa 14

**2022 utatue balaa taka za plastiki, kielektroniki**

TEKNOLOJIA
NA MWANDISHI WETU

# 2021 imeandika historia MNH kupandikiza uloto

TEKNOLOJIA ya kupandikiza uloto kwa wagonjwa wa saratani ya damu ni utaalamu mpya ulioanza kutumika nchini Novemba 2021, kwa Hospitali ya Taifa Muhimbili, ni kuandika historia kufanikisha kuokoa maisha ya wagonjwa wa saratani ya damu.

Mara nyingi kama si zote, saratani ya damu ilichukuliwa kama hukumu ya kifo kwa vile maradhi hayo, yalidhoofisha mwili na kuukaushia damu, lakini sasa historia imebadilishwa.

Utaalamu huo unaohusisha kuondoa seli zote za saratani kwenye viwanda vya kutengeneza damu mwilini katikati ya mifupa kitaalamu inafahamika kama 'bone marrow transplant,' anasema Daktari Bingwa wa Magonjwa ya Damu, Dk.Stella Rwezaula kutoka Hospitali ya Taifa ya Muhimbili.

Dokta Stella Mkuu wa Idara ya Hematolojia ya Hospitali ya Muhimbili, anafafanua kuwa saratani ikiwa kwenye damu, inamaanisha mwili mzima una seli za kansa kwa sababu uhai wa binadamu uko kwenye damu inayohusika na kusafirisha hewa safi na kuondoa chafu, kusambaza chakula, maji na michakato yote ya maisha .



Mashine ya mionzi moja ya tiba za kusaidia wagonjwa wa saratani. **PICHA: MTANDAO**

### KAZI YA KUPANDA ULOTO

Kwa hiyo kinachofanyika ni kuua seli zote mwilini ambazo ziko ndani ya damu, mfano chembe nyeupe, nyekundu, sahani na chembe mama (stem cells) za aina mbalimbali, anasema Dk. Stella.

Anasema tiba huanza kwa kuwapa wagonjwa dawa za kutibu kansa kwenye damu, akikumbusha kuwa kila aina ya saratani ina dawa yake maalumu au 'chemotherapy' inatamkwa 'kemotherapi' inayotolewa kama vidonge, sindano au dripu na kwa saratani ya damu anapewa 'kemo'kwa miezi minne hadi sita.

Anaongeza kuwa, baada ya hatua hiyo mgonjwa akishapona kabisa, kinachofuata ni kupandikiza uloto kwa kutumia teknolojia mpya ambayo mwenye kuchangia uloto analazwa na kupewa dawa inayosimamia uzalishaji wa seli kuu (stem cells) za damu ili zipatikane kwa wingi kwa wakati mfupi ili kuzihamishia kwa mgonjwa wa kansa.

"Mchangia uloto analazwa na kuingizwa kwenye mashine ya spectra Optia, ina upande mmoja unatoa damu mwilini na kukusanya seli mama stem cells) na upande mwingine unarudisha damu mwilini, iliyochambuliwa na kuondolewa mama ni kazi inayofanywa kwa saa nne hadi sita na hizo seli kuu zinakusanywa kwenye mifuko ya damu kama ile inayotumika kukusanya au kuhifadhi damu salama," anafafanua mtaalamu.

Baada ya kukusanya damu yenye seli mama hizo kutoka kwa mchangiaji , mgonjwa anaanza tiba kwa kupewa dozi kubwa ya dawa za saratani (kemotherapi), ili kumaliza seli za kansa zilizojificha popote mwilini mfano kwenye mishipa ya fahamu na ubongoni.

Dokta Stella, anasema baada ya tiba hiyo mgonjwa anapewa damu hiyo yenye stem cells mpya kwa njia za kawaida zinazofanyika kwenye kuongeza damu na uloto mpya huanza kuota ndani ya mifupa na kuzalisha damu kati ya wiki mbili hadi tatu tangu aliposafishwa na kuwekewa huo mpya.

Usipoota inakuwaje? Akijibu swali hilo anasema mara nyingi unaota na ufafanuzi zaidi ni kwamba, tiba hiyo inatolewa kwa wagonjwa wa saratani ya damu inayoitwa 'acute leukemia' ambayo inashambulia chembe mama changa (immature stem cells) kwa wenye kansa inayoshambulia chembe mama za kuzalisha damu zilizokomaa.

Anasema, kwenye saratani inayoshambulia 'immature stem cells,' mgonjwa anapewa uloto wa mchangiaji ambao unabadilisha kundi la damu yake iwapo alikuwa na kundi A la damu, anapopitia michakato yote ya kutibu saratani, iwapo uloto mpya ulitolewa na mwenye damu kundi 'O' hubadilika kuwa kundi O.

Ni wagonjwa wangapi waliotibiwa? "Hadi sasa Muhimbili imebadilisha na kupandikiza uloto wagonjwa watano, ni teknolojia inayomwezesha mgonjwa kuendelea kuishi na kuongeza miaka zaidi licha ya kushambuliwa na kansa." Anasema anapoulizwa iwapo kupanda uloto kunaondoa kansa mwilini.

Akizungumzia suala la gharama, anasema ni kubwa ikifikia kati ya Shilingi milioni 250 hadi 300 iwapo tiba itafanyika nchini India na kwamba kwa upande wa Muhimbili inapungua mno na kugharimu shilingi milioni 70 na kwamba mgonjwa akiwa na bima ya afya, inachangia kupunguza baadhi ya gharama za matibabu kwa mgonjwa.

Anafafanua kuwa teknolojia hiyo ya kupanda uloto inatumiwa pia kutibu saratani ya mitoki,lymphoma, matatizo ya selimundu na hata wagonjwa ambao uloto wao hauzalishi seli mama za damu na walioathirika na saratani zinazoshambulia seli nyeupe na mfumo wa kinga ya mwili.

ELIMU

NA SABATO

KASIKA

KULENGA VITA UVIKO 2021

# 2022 ulete kasi, ari ,nguvu mpya viongozi, jamii waache mazoea



Eneo lililokuwa likitumiwa na machinga Mbezi Mwisho Dar es Salaam, likiwa wazi baada ya serikali kuwaondoa. **PICHA: SABATO KASIKA**

TUNAWAPENDA na kuwatakia kila la heri wasomaji wa kijarida chetu cha TESA heri ya Mwaka Mpya wa 2022. Tukiwakumbusha kujikinga na UVIKO 19. Zaidi tunawakaribisha tena kuendelea kuwa nasi. Nakala yetu hii ndiyo ya mwisho kwa mwaka 2021, ambao unaelekea ukingoni baada ya safari ndefu ya miezi 12 yenye matukio mbalimbali likiwamo la serikali kufanikiwa kuhamisha machinga kwenye maeneo yasiyo rasmi na kuwapeleka katika masoko.

Ni mara ya kwanza zoezi hilo kufanikiwa, kutokana na kwamba kila serikali ilipojitahidi kuwaondoa ilikutana na vikwazo, vikiwamo kutoka kwa watu mbalimbali kama wanasiasa, baadhi yao waliwatetea kutokana na maslahi yao binafsi, hali iliyosababisha hata machinga wenyewe kugoma kuhama hali ambayo wakati mwingine ilichochea vurugu kati yao na vyombo vya dola.

Tofauti na miaka mingine, safari hii machinga wamehamishwa bila kutokea vurugu za aina yoyote licha ya changamoto hizo ni za baadhi ya machinga kurudi kwenye maeneo ya awali wakati wa jioni, kwa maana kwamba wanavizia muda huo wakijua kuwa hakuna wa kuwafukuza ndipo wanapanga biashara zao.

Mbinu zilizotumika kufanikisha machinga kuondoka maeneo ya awali katika mikoa mbalimbali nchini, zingetumika pia kwenye kuhamasisha umma wa Watanzania kuwa makini dhidi ya maambukizi ya corona.

> **Maambukizi ya ugonjwa ugonjwa huo yanaongezeka huku ukiendelea kuhimiza wananchi kuchukua tahadhari ambazo zinaweza kusaidia kuepuka kukumbwa na UVIKO-19.**

Ni vyema hatua zaidi za kukabiliana na ugonjwa huo zitumike, kutokana na kwamba watu wanaendelea na shughuli zao kama kawaida bila kujali afya zao, hali ambayo inaweza kusababisha wakapata ugonjwa huo.

### HALI IKOJE?

Pamoja na kuwapo miongozo, bado kuna baadhi ya watu hawachukui hatua zozote zitakazowawezesha kuwa salama dhidi ya ugonjwa, kwani wanaovaa barakoa ni wachache au wakati mwingine hakuna anayevaa. Hasa kwenye mabasi, maeneo ya ibada wakati mkazo unakuwa hospitalini zaidi.

Mojawapo ya maeneo hayo ni stendi za mabasi zikiwamo za daladala na ya mikoani, ambako watu wanakusanyika bila tahadhari, na pia ndani ya daladala, abiria wanajazana, huku wakiwa hawajavaa barakoa.

Iwapo mtu akipata nafasi ya kutembelea Mbezi Luis Dar es Salaam, kuanzia stendi za daladala na hata ya mabasi ya mikoa ya Magufuli atashuhudia hali hiyo kwamba bado kuna msongamano mkubwa wa watu wasiochukua tahadhari.

Siyo stendi pekee bali hata kwenye masoko ya eneo hilo, hayana ndoo za maji tiririka, watu wanaendelea na shughuli zao kama kawaida wakiwamo wafanyabiashara na wateja wao.

Kwa mazingira kama hayo, ni wazi kwamba unahitajika utashi wa kisiasa kwa ajili ya kuhakikisha watu wanachukua tahadhari ambayo itawasaidia kuepuka ugonjwa wa corona ambao unaendelea kuangamiza watu duniani.

Ingependeza kama mwaka ujao ukiwa wa Watanzania kuchukua hatua zinazotakiwa kwa ajili ya kuepuka ugonjwa huo badala ya watu kusubiri kusukumwa kulinda afya zao.

### MAELEKEZO

Licha ya serikali kutoa mwongozo wa udhibiti corona kupitia afua ya kuthibiti misongamano katika jamii bila kuathiri shughuli za kiuchumi toleo la kwanza ambao unaweka wazi jinsi ya kujikinga na ugonjwa huo, hakuna ufuatiliaji wala kusimamia endapo unatekelezwa.

Mwongozo huo unataka kila mtu kuvaa barakoa katika vyombo vya usafiri na stendi za mabasi, daladala na bodaboda, huku vyombo vya ulinzi na usalama vikitakiwa kusimamia utekelezaji wa mwongozo huo.

Unagusa pia kwenye vituo vya mabasi, ambako wasafiri wanatakiwa kunawa hivyo kuwepo na ndoo za maji tiririka ili abiria wapate huduma hiyo kabla ya kupanda ndani ya vyombo vya usafiri huku wakiwa wamevaa barakoa, lakini yote hayo hayapo.

Mwongozo huo unahimiza wananchi kuepuka mikusanyiko isiyo ya lazima, lakini vyombo vya usafiri kama daladala na mabasi ya mikoani kuzingatia idadi ya viti kwa kutojaza abiria kupita kiasi.

Hivyo ndivyo vita dhidi ya corona imekuwa ikifanywa, huku utoaji wa chanjo nao ukiendelea kwa lengo la kulinda afya za Watanzania ingawa inaonekana baadhi ya watu ni wagumu kuchukua hatua na hakuna viongozi wanaofuatilia na kuhakikisha utekelezaji.

Mwaka huu uanze na usimamizi na ufuatiliaji kama ambavyo mwongozo unaelekeza vyombo vya usalama kusimamia suala hilo kwenye vituo vya mabasi ili kila anayesafiri ahakikishe amenasa na amevaa barakoa.

Hatua hiyo inaweza kusaidia, ili asiyenawa na asiyevaa barakoa, azuiwe kupanda basi la abiria hadi hapo atakapozingatia maelekezo ya mwongozo, lengo likiwa ni kusaidia kupunguza maambukizi ya ugonjwa huo nchini.

Wizara ya Afya inasema, maambukizi ya ugonjwa ugonjwa huo yanaongezeka huku ukiendelea kuhimiza wananchi kuchukua tahadhari ambazo zinaweza kusaidia kuepuka kukumbwa na UVIKO-19.

Kwa mujibu wa Waziri wa Afya, Dk. Dorothy Gwajima, idadi nyingi ya sampuli zinazopokewa katika Maabara Kuu za Taifa zimeongezeka kutoka 14 kwa siku hadi kufikia 47 kwa siku, hali inayoonyesha idadi ya maambukizi inaongezeka.

Hivyo, si vibaya mbinu zilizotumika hadi machinga wa mikoa mbalimbali nchini wakahama bila vurugu, zingetumika kukabiliana na ugonjwa huo, kwa maana kwamba wasiozingatia mwongozo wachukuliwe hatua.

Maeneo yote yenye mkusanyiko wa watu, yangekuwa na maji tiririka kila mmoja anawe na avae barakoa, asiyefanya hivyo asipewe huduma iwe ya usafiri au nyingine kulingana kile anachohitaji.

Kwa njia hiyo ikiwamo pia ya kupata chanjo, inaweza kuwa rahisi kukabiliana na ugonjwa huo na kufanikisha kudhibiti kirusi cha omicron kilichojiongeza zaidi na hivyo kila mmoja kuchukua hatua ikibidi kushurutishwa na kutozwa faini, kama ilivyo kwa wamachinga.

ELIMU
NA CHRISTINA MWAKANGALE

KAZI za ubunifu wakati mwingine ni lazima ziendane na mazingira ndiyo maana leo wakazi wengi wa mikoa ya joto kama Dar es Salaam wangetamani yapatikane mabati ya gharama nafuu yanayobadilika na kutengeneza hali ya ubaridi msimu huu wa jua na joto kali.

Bati la paa linalozalisha ubaridi wakati wa jua lingekuwa mbadala wa feni na viyoyozi yote hayo yakilenga kutatua changamoto zinazofanana na mazingira ya Watanzania.

Mfano wa ubunifu wa kifaa cha kuvuna sumu ya nyuki wa Tanzania kilichobuniwa na watafiti hivi karibuni ni moja ya kazi zinazoakisi hali ya mazingira.

Kifaa hicho cha kupata sumu ya nyuki kinaundwa na vijana wahitimu wa Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam (DIT), Theresia Sembua na Patrick Kitosi, wanaosema wanafanya hivyo wakiamini kuwa sumu hiyo ina soko ndani na nje ya nchi na kama wafuga nyuki wakiipata na kuiuza wanaweza kuleta mabadiliko kiuchumi kifamilia na kitaifa.

Sumu ya nyuki au 'bee venom' hutumika zaidi kwa ajili ya tiba, dawa na hata kwenye vipodozi kwa ajili ya kutibu ngozi pamoja na majeraha ya moto au vidonda.


Theresia alisema hayo alipozungumza na Nipashe hivi karibuni akitaja mikakati ya namna jamii inavyoweza kugeukia fursa zenye tija kubwa kiuchumi wakati wa mkutano uliowakutanisha wanaharakati ngazi ya jamii kutoka vituo tofauti ikiwamo Mabwepande, Saranga, Majohe na Kivule mkoani Dar es Salaam, iliyoandaliwa na Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP).

Anabainisha kuwa kifaa hicho kinachovuna sumu ya nyuki, ambacho huwekwa jiirani na mzinga msituni, kinaendana na mazingira ya nyuki wa hapa nchini na kinaundwa kwa gharama nafuu, akiendelea kusema:

"Ni ubunifu mpya katika mazingira mapya ya huku Afrika. Kitu ambacho kimetusukuma kufanya utafiti huu ni kwamba nyuki wanatabia ya kubadilika badilika kutokana na mazingira ya hali ya hewa. Mimi ni sehemu ya utafiti huo ambao tunashirikiana na mwenzangu tukifanyia kazi pamoja."

"Nyuki wa Ulaya au China, ni tofauti na nyuki wa Afrika na Tanzania pia, wa hapa nchini hata nao hutofautiana ,nyuki wa Tabora wanakuwa na tabia tofauti na wa Pwani, kwa hiyo huwezi kuchukua mashine kutoka China ukaitumia kuvuna sumu hii kwa nyuki wa hapa nyumbani ukaipata kwa ufanisi," anasema Theresia.

Anasema sumu hiyo inayopatikana kutoka kwenye nyuki inauzwa sehemu mbalimbali duniani na iwapo itakusanywa kwa wingi inauzwa kati ya Shilingi 150,000 hadi 300,000 kwa gramu moja na kwamba kifaa hicho kimeshafanyiwa majaribio ya awali na kuonyesha ufanisi.



Kifaa cha kunasa sumu ya nyuki kinachofaa na kuendana na mazingira ya Tanzania. **PICHA: CHRISTINA MWAKANGALE**

# Wasomi walioibuka na kinasa sumu ya nyuki

> **Ni ubunifu mpya katika mazingira mapya ya huku Afrika. Kitu ambacho kimetusukuma kufanya utafiti huu ni kwamba nyuki wanatabia ya kubadilika badilika kutokana na mazingira ya hali ya hewa.**



"Tumekitengeneza kwa teknolojia ya kielektroniki ikimaanisha kuwa inaundwa kama kompyuta na inatoa shoti ya umeme na inapowagusa wanashtuka na wakasirike na kutoa sumu yao, na kumwagika kwenye sehemu maalumu ya kifaa hiki ili kukusanywa na wafugaji hao."

## UMUHIMU WAKE

Theresia anasema sababu ya kubuni kifaa hicho ni baada ya kutafiti na kubaini kazi ya sumu hiyo na matokeo ya soko na mahitaji kwenye jamii hasa kwa vile hutibu magonjwa ya mishipa ya fahamu, misuli kukakamaa, baridi yabisi, magonjwa ya ngozi, pumu, mzio vilevile kutengenezea vipodozi na chanjo mbalimbali.

Kadhalika, anabainisha kuwa ina matumizi mengi hasa ya afya kama kuzalisha dawa na kinga dhidi ya mangojwa na katika baadhi ya viwanda hutumiwa kutengenezea vipodozi vya ngozi, ambavyo vinarekebisha ngozi (serum) iliyoanza kuzeeka, au yenye michubuko na mikwaruzo.

Akifafanua kuhusu sumu hiyo sokoni anasema huuzwa kwa wastani wa Shilingi 150,000 hadi 300,000 kwa gramu moja kutegemeana na ubora pamoja na eneo ilikovunwa.

Sehemu inakouzwa sumu hiyo, anasema ni katika maabara mbalimbali za utafiti wa dawa pamoja na hospitali kubwa na kwamba anafahamu hutumika pia kwenye Taasisi ya Utafiti wa Dawa za Binadamu (NIMR) kutengeneza tiba zinazokusudiwa.

"Baadhi ya mikoa yenye watu wanaozalisha sumu hiyo na Tabora , Singida na Dodoma na inawezekana kabisa kila mrina asali au wafuga nyuki, wakaamua kuwa na kifaa hiki ili kuvuna sumu hii. Ndilo jambo kubwa lililotusukuma kufanya utafiti huu ili kumsaidia mkulima wa hapa Tanzania kupata kifaa hiki kilichotengenezwa maalumu kwa ajili ya mazingira ya humu nchini."

## UTAFITI WAITHIBITISHA

Utafiti uliofanywa kwa wiki 12 kwa wanawake 22 waliopaka mafuta yenye 'serum' ya mchanganyiko wa sumu ya nyuki mara mbili kwa siku, ulibaini kuwa walipunguza makunyanzi usoni, ikilinganishwa na bidhaa nyingine ambazo zilitumiwa awali bila matokeo hayo, anasema Theresia.

Pia kwa wiki sita baadae watu wengine ambao walitatizika na ngozi hasa chunusi usoni ambao kwa asilimia 77 walitumia mchanganyiko wa mafuta yenye sumu ya nyuki,walipata matokeo mazuri, anaongeza.

Vilevile, kampuni nyingi za kuutunza ngozi zimeanza kuongeza sumu ya nyuki kwenye bidhaa kama vile serum na vimiminika baada ya kubaina kuwa kiambato hicho kinaweza kukuza afya ya ngozi kwa njia kadhaa, ikiwa ni pamoja na kupunguza uvimbe, kutoa vimelea na athari zake.

Anasema ushahidi kutoka kwenye utafiti wa wanyama unapendekeza kuwa tiba ya sumu ya nyuki, inawezakupunguza dalili za hali ya kushuka kingamwili, na kinga kuushambulia mwili kama vile 'lupus, encephalomyelitis.'

Utafiti umeonyesha kuwa matibabu haya ni salama na yanafaa na yanaweza kupunguza hatari ya baadaye ya athari mbaya za kutumia dawa kwa muda mrefu.

ELIMU

NA MWANDISHI WETU



Taka za plastiki zinazojaza bahari, mito na maziwa ni chanzo cha vifo vya viumbemaji. Kasa akihangaika kwa mateso ya kunaswa baada ya kuzongwa na nyavu baharini. **PICHA: MTANDAO**

# 2022 utatue balaa taka za plastiki, kielektroniki

MWAKA 2021 umeondoka karibu 2022. Tunawatakia kila la heri wasomaji wetu wa TESA na zaidi heri ya mwaka mpya unaosherehekewa Jumamosi wiki hii.

Ujio wa mwaka mpya kimazingira unakutana na changamoto kubwa kitaifa ambayo inahitaji wataalamu kung'amua namna bora ya kutupa na kurejeleza taka za plastiki na za kielektroniki.

Plastiki zinaendelea kuwa taka ngumu zisizodhibitika zimejaa kila mahali kuanzia mashambani, kwenye viwanja vya shule na maeneo ya wazi, mitaroni na barabarani.

Mwisho wa taka hizo ni kwenye vyanzo vya maji kama mtoni, ziwani na baharini. Hivyo elimu ya kuhifadhi taka hizo na namna ya kuzichakata ni suala linalohitaji kipaumbele.

Lengo namba 14 la maendeleo endelevu linazungumzia maisha na rasilimali za majini zinazohusu bahari, maziwa na mito. Vyote hivyo hapa nchini vinajaa plastiki.

Iwapo samaki na chumvi zinazovunwa kutoka baharini vinaathirika na plastiki ni wazi hatma ya watu wanaokula vitu hivyo iko shakani.

Plastiki kuanzia matairi ya aina zote, vyombo vya nyumbani, vifaa vya kielektroniki na aina zote za vifungashio zikiwamo chupa za vinywaji mbalimbali zinaishia majini.

Ni dhahiri samaki watakula, wataumia na mwishoni watatoweka. Mazalia yao chini ya mikoko, kwenye delta na madimbwi yatafunikwa na plastiki na mayai yatakayoanguliwa hayawezi kuishi kwenye plastiki, mwisho maisha ya viumbe majini yatakoma maeneo hayo kubaki tupu.

### HATUA ZA MUHIMU

Janga la plastiki ni kubwa na p engine ni wakati wa kuzibana kisheria kampuni zinazozalisha bidhaa za plastiki kuanzisha viwanda vya kurejeleza mabaki yake.

Hatua hiyo inaweza kuwa ya njia mbalimbali mfano kuhusika moja kwa moja kuanzisha viwanda hivyo, kushirikiana na wadau zikiwamo halmashauri za miji na majiji pamoja na wawekezaji wengine, lakini kikubwa kuwe na udhibiti.

Pamoja na viwanda ni vyema wawekezaji hao wakaanzisha , vituo vya kisasa vya kukusanyia vifungashio vyao iwe chupa, viti, au mabaki mengine ya taka hizo ili iwe rahisi kwa wajasiriamali kuvifikia baada ya kuzikusanya ili vipelekwe viwandani kwa utaratibu unaoeleweka.

Pamoja na kushiriki kuanzisha viwanda vya kurejeleza watafiti wa vyuo vikuu na taasisi za teknolojia na ufundi zishauri aina za bidhaa zinazoweza kupatikana kupitia urejelezaji.

> **Kwa ujumla bunge lifikirie kutunga sheria za kuwabana wanaoingiza mitumba ya viwango duni kwa vile hata vyombo vya nyumbani vya plastiki huuzwa nchini.**

Aidha, wataalamu na watafiti waeleze mbinu nyingine ya kudhibiti na kuharibu taka za plastiki kwa gharama nafuu , isiwe ni kurejeleza wakati wote na hilo lilenge kuwasaidia wakazi wa vijijini. Cha msingi ni kuhamasisha watu kutunza mazingira na kudhibiti plastiki lakini pia taifa kuwa na sheria na kuweka miongozo ya kudhibiti utupaji plastiki ovyo unaoendelea sasa.

Kila kampuni inayozalisha au kuhusika na plastiki iajiri mtaalamu mshauri na mikakati ya kudhibiti taka hizo na kuwasilisha ripoti na kazi zake NEMC ili zikaguliwe na kufuatiliwa.

### TAKA ZA KIELEKTRONIKI

Mabaki ya viambato vya bidhaa za kielektroniki kama simu, betrii zake, mifuniko, halikadhalika kompyuta , betrii zake ni kitisho kingine kwa mazingira .

Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC), lifuatilie na kusimamia udhibiti wa taka za plastiki na za kielektroniki ili kuikoa nchi na janga la ardhi, maji na mimea kujaa madini tembo (heavy metals) kama chuma, nikel, zebaki, shaba, kromiam, cobalt na manganizi ambavyo hutumiwa kutengeneza simu hizo na vifaa vingi vya kielektroniki.

Madini tembo yanatajwa kuwa ni chanzo cha saratani.

### KUONDOA BIDHAA MITUMBA

Tanzania kwa miaka mingi imeruhusu kuingizwa na kuuzwa bidhaa 'bandia' au 'cheap' au duni na hafifu kwenye soko lake.

Bidhaa hizo kutoka nchi za Asia kwa mfano mwavuli unaochakaa na kutupwa pale tu unapofunguliwa, nyingine ni miswaki ikiwekwa midomoni brashi zote zinang'oka lakini pia kuna vijiko vinavyopata kutu hata kabla ya kutumiwa.

Aina mbalimbali za 'toi' kama magari, ndege, kompyuta, bastola na za wanyama ni bandia, ikitumiwa baada ya saa chache inavunjika wakati gari au ndege halitembea wala kuiruka kwa vile betrii yake ni duni au haina kiwango. Kadhalika wanyama nao hawatembei na kinachofuatwa ni kutupwa na kuongeza taka za plastiki mitaani.

Simu nazo ni balaa zimejaa kila mahali. Licha ya kuwa na jina na lebo za kampuni za kimataifa, si simu ni kama 'toi' hazidumu.

Spika zake ni mbovu, haitosi sauti, wala hazisikiki, chaja yake inakufa baada ya kuiweka kwenye umeme kwasababu haipeleki moto.

Nyingine hata kama inapeleka moto betrii yake haichaji inashinda na kulala kwenye umeme lakini haiingii chaji. Baada ya muda betrii inatuna, inatumiwa bila mfuniko na baada ya wiki chache inatupwa.

Simu hizo ndizo zinazonunuliwa na Watanzania walio wengi kwa sababu ni bei ndogo kuanzia Shilingi 15,000 hadi 25,000.

Ili kumalizana na changamoto hizo, taifa linahitaji kufikiria ni kuandaa sheria ya kuzuia na kupiga marufuku uingizaji bidhaa 'cheap', duni, zisizo na kiwango ili kulinda afya ya watu na mazingira yao.

Hatua hiyo ni muhimu kwa sababu vitu hivyo vinaingiza mamilioni ya tani za taka za 'sumu' na hatarishi kuanzia betrii na viambato vya simu kwenye maji, ardhi na kuzidi kuchafua mazingira.

Kwa ujumla bunge lifikirie kutunga sheria za kuwabana wanaoingiza mitumba ya viwango duni kwa vile hata vyombo vya nyumbani vya plastiki huuzwa nchini.

Bidhaa kama friji, TV, vyerehani, redio, toi kama pikipiki, baiskeli, magari na kamera za mitumba zilizopitwa na wakati zinaruhusiwa kuingizwa nchini ili nini? Mbona baada ya muda wanunuzi watalazimika kuvitupa.

Ni vyema NEMC kamati za mazingira, bunge, vyama vya elimu ya juu, watafiti na asasi za kiraia zikafuatilia na kusaidia kupata mbinu za kudhibiti , kwa vile kama taifa halitaziba ufa litajenga ukuta.

# Vifo watoto wachanga, wajawazito vyapungua

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

MGANGA Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Dk. Best Magoma, amesema pamoja na vifo vya watoto wachanga na wajawazito kupungua mkoani hapo jitihada zinahitajika kukabilina na tatizo hilo.

Dk. Magoma alibainisha hayo alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari jijini hapa kuhusu hali ya vifo vya wachanga pamoja na wajawazito kwa mkoa huo.

Alisema katika kipindi cha mwaka 2020 vifo vya wajawazito vilikuwa 88 na hadi kufikia mwezi Novemba mwaka huu idadi hiyo imeshuka hadi 64.

"Kuna maendeleo chanya ya vifo hivi kupungua kwani hata vifo vya watoto wachanga vimepungua kutoka 690 mwaka 2020 hadi kufikia 529 mwezi Novemba mwaka huu, tumejielekeza vifo hivi kupungua hadi kufikia asilimia 25 kwani idadi bado kubwa sana,

"Bado tuna kazi ya kufanya kwetu sisi hata kifo kimoja kwetu kina maana tunahitaji kufanya kwa pamoja ili kuboresha huduma ya afya," alisema Dk. Magoma.

Alisema sababu ya vifo hivyo ni pamoja na kutokwa na damu nyingi kwa wajawazito wakati wa kujifungua, kifafa cha mimba, watoto kupata maambukizi kabla na wakati wa kujifungua pamoja na uzito mdogo.

"Jitihada ngazi ya familia, jamii inahitajika lazima tushirikiane wote ili mikakati hii tuliojiwekea iweze kusaidia kumaliza hali hii," alisema Dk. Magoma.

Akizungumzia hali ya magonjwa katika mkoa huo, Dk. Magoma alisema katika kipindi cha kuanzia Julai 2021 hadi Novemba 2021, hakukuwa na ugonjwa wowote wa mlipuko.

"Hata hivyo, kwa kipindi hiki mkoa na taifa kwa ujumla kumekuwa na tahadhari ya kuwapo kwa mlipuko wa ugonjwa wa homa ya mapafu unaosababishwa na virusi vya corona," alisema.

Alisema mkoa kupitia timu ya usimamizi wa huduma za afya umeendelea kuchukua tahadhari za kujikinga na maambukizi ya ugonjwa wa UVIKO-19.

Akizungumzia vituo vya kutolea huduma za afya, alisema mkoa una jumla ya vituo 447 vya kutolea huduma hizo zikiwamo hospitali 16, vituo vya afya 47, zahanati 373, kliniki nane vituo tisa vya kungojelezea wajawazito na cha uchunguzi.

## Wanachama CHF sasa kuchangia kielektroniki

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

SERIKALI imezindua mfumo wa kielekitroniki wa kukusanya michango ya wanachama wa CHF iliyoboreshwa ambao kwa sasa una wanachama zaidi ya milioni moja.

Akizungumza katika mafunzo rejea ya siku tatu ya matumizi ya mfumo huo wa kielekitroniki kwa timu za uratibu wa mfuko wa CHF iliyoboreshwa hivi karibuni, Kaimu Mkurugenzi Msaidizi wa Huduma za Afya, Ustawi wa Jamii na Lishe katika Ofisi ya Rais – TAMISEMI, Rasheed Maftah, aliwaelekeza kufanya mafunzo rejea ya matumizi ya mfumo huo kwa timu za uratibu wa CHF iliyoboreshwa za halmashauri, wasimamizi ngazi za kata na maofisa Waandikishaji/ Mawakala ngazi za vijiji/mitaa kabla ya Januari 10, 2022.

Mafunzo hayo yalishirikisha Waratibu wa CHF-iliyoboreshwa katika ngazi ya mkoa, maofisa TEHAMA na timu za CHF za halmashauri kutoka nchi nzima.

Pia, Maftah alisema timu hizo zinatakiwa utekelezaji wa matumizi ya mfumo wa kielekironiki katika kukusanya michango ya wanachama ifikapo Januari 15, 2022. "Ofisi ya Rais - Tamisemi, inaishukuru Wizara ya Fedha na Mipango (MoFP) na wadau wa maendeleo HPSS- Tuimarishe Afya kwa kufanikisha kukamilika kwa mfumo huu utakaowezesha ukusanyaji wa michango ya wanachama wa CHF iliyoboreshwa kielektroniki uliounganishwa na Mfumo wa "Government e-Payment Gateway System (GePG)", alisema Maftah. Serikali imekuwa ikisisitiza matumizi ya mifumo ya kielektroniki ya ukusanyaji na usimamizi wa fedha za umma.




Spika wa Bunge, Job Ndugai (katikati) akizungumza wakati wa kufungua mkutano mkuu wa kabila la Wagogo (Wanyausi) uliofanyika mwisho wa wiki Jijini Dodoma. Kulia ni katibu wa kikundi hicho,Amon Chipalo na kushoto ni Mwenyekiti wake ,Grace Lesilwa .**PICHA IBRAHIM JOSEPH**

# Ndugai ataka wananchi kuwekeza walipozaliwa

**Na Ibrahim Joseph,** DODOMA

SPIKA wa Bunge, Job Ndugai amewataka wananchi wenye uwezo kiuchumi kuwekeza kwenye maeneo walipozaliwa ili kutoa fursa za ajira kwenye maeneo hayo.

Alitoa wito huo mwishoni mwa wiki alipokuwa akizungumza kwenye mkutano mkuu wa kabila la Wagogo uliofanyika jijini hapa.

Aliwataka watu wenye uwezo kifedha kuwekeza kwenye maeneo yao ya asili waliyozaliwa ili kutoa fursa za ajira kwa wananchi wa meneo hayo.

"Nawashukuru viongozi walioitisha mkutano huu, lakini lazima tuelezane ukweli wale wenzetu waliofanikiwa kiuchumi tunatakiwa kuwekeza nyumbani ili kutoa fursa za ajira kwa wenzetu walipo maeneo hayo," alisema.

Aliitaka jamii za watu hao wanaoishi nje ya maeneo yao ya asili kutembelea kwao ili kuangalia fursa za uwekezaji zilizopo katika maeneo hayo.

Kadhalika, aliwataka wasomi kusaidia jamii za maeneo waliyotoka ili kuwavutia wengine kupenda elimu.

"Siku hizi elimu inawagombanisha wazazi na wahitimu wa elimu ya juu kwa sababu hawaoni tofauti ya wasomi na wengine walioachwa vijijini," alisema.

Alisema wakati mwingine wenye elimu ndogo wamekuwa na msaada mkubwa kwenye familia kuliko wale wenye elimu ya juu na kuleta shaka juu ya uwezo wao.

Aliongeza kuwa wasomi hao wanatakiwa kujitolea kutoa elimu kwa jamii iliyopo kwenye maeneo yao ili iweze kunufaika na uwepo wao. Vile vile, alisema matarajio ya mkoa wa Dodoma ni kuingia kwenye kundi la kumi bora kielimu kwenye msimu ujao wa mwaka 2022.

Alisema mkoa umejipanga kwa kuwatumia wasomi na kuwahamasisha wazazi kuwasaidia watoto wao kupenda masomo na sasa hakuna utoro shuleni na wanafunzi pamoja na walimu wanaendelea kuchapa kazi kunakochangia ufaulu kuongezeka zaidi.

Mwenyekiti wa kikundi cha Wagogo, Grace Lesilwa, alisema matarajio ya kikundi chao ni kujenga makumbusho ya kabila hilo katika kijiji cha Mchemwa.

Lesilwa alisema lengo la makumbusho hayo ni kuendeleza mila na desturi za kabila hilo pamoja na kuweka kituo cha utalii kitakachotangaza vivutio vya utalii vilivyopo mkoa huo.

Aliishukuru serikali kwa kuhamishia makao makuu yake mkoani hapo ambayo yametoa fursa za ajira kwa wazawa na wananchi wake.

Katibu wa kikundi hicho, Amon Chipalo, alisema mkutano huo uliwakutanisha Wagogo waishio mikoa mbalimbali na wengine kutoka nje ya nchi.

Chipalo, alisema malengo ya umoja huo ni kusaidia katika nyanja ya elimu kwa kujenga vyumba vya madarasa kuchangia sekta ya maji, kilimo na mazingira.

Alisema hayo yote yatafanikiwa kwa kuwatumia wazawa wa kabila hilo pamoja na kuwashirikisha wadau wengine wa maendeleo wa ndani na nje ya nchi.





# Wanafunzi 150 wasaidiwa vifaa vya shule

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

MBUNGE wa Jimbo la Mbeya Vijijini, Oran Njeza ametoa vifaa vya shule kwa zaidi ya watoto 150 wanaoishi na maambukizi ya Virusi vya Ukimwi (VVU) ambao wanalelewa katika Hospitali Teule ya Wilaya ya Mbeya ya Ifisi chini ya Kitengo cha Ustawi wa jamii.

Alitoa vitu hivyo pamoja na sukari kwa ajili ya kundi hilo mwishoni mwa wiki alipojumuika na watoto hao pamoja na walezi wao ikiwa ni sehemu ya kulifariji katika kipindi hiki cha Sikukuu za mwisho wa mwaka. Vifaa alivyokabidhi ni pamoja na madaftari, peni, kalamu za risasi na rula ambavyo vimegawanywa kulingana na madarasa ya watoto hao kuanzia wanaotarajia kuanza darasa la kwanza mpaka wanaojiunga na vyuo mbalimbali nchini.

Alisema kitendo cha watoto hao kujumuika pamoja kinawapa nafasi ya kupata elimu sahihi kuhusu maambukizi ya VVU na namna ya kuishi na virusi hivyo bila kudhoofika afya wala kupoteza maisha.

Njeza aliwapongeza wazazi na walezi wa watoto hao kwa kuamua kuwaruhusu kujumuika kwenye umoja huo ujulikanao kwa jina la Teen Club ambao unawasaidia kupata elimu ya pamoja na kuhamasishana kuwa wafuasi wazuri wa dawa.

"Kilichonifurahisha ni kwamba nyie mnajitambua, wazazi wenu wanajitambua na hata dada zenu na kaka zenu wanajitambua, wapo baadhi ya watu wanaishi na VVU, lakini hawataki kabisa kujionyesha kama ninyi, hongereni sana na naamini mnapata malezi sahihi," alisema Njeza.

Aliupongeza uongozi wa Hospitali ya Ifisi pamoja na uongozi wa Halmashauri ya Mbeya kwa kushirikiana kuwalea watoto hao akisisitiza kuwa mpango huo ni sahihi kwa ajili ya kuokoa maisha ya watoto hao pamoja na watu wengine wanaoishi na maambukizi.

Msimamizi wa kituo hicho, Dk. Khamis Bakari, alisema kituo hicho kilianzishwa mwaka 2017 kikiwa na watoto 25, mpaka sasa kina zaidi ya watoto 150 wa umri tofauti na ngazi tofauti za elimu.

Alisema huduma hizo zilianzishwa na serikali mwaka 2015 kwa lengo la kupunguza vifo vya watoto vitokanavyo na virusi vya Ukimwi kwa kuhakikisha watoto hao wanapata huduma sahihi ikiwamo kutumia dawa za kufubaza virusi.

Alisema watoto hao hukutana kila mwisho wa mwezi kwa ajili ya kupata elimu sahihi ya namna ya kuishi na VVU na yapo malengo ambayo wanayatekeleza kwa kushirikiana na wadau mbalimbali.

"Lengo letu ni kuhakikisha watoto hawa wanafikia malengo yao ya kimaisha ikiwamo kufanya vizuri kwenye masomo, lakini tatizo ambalo huwa linatokea ni baadhi yao kushindwa kufanikisha malengo yao kutokana na kukosa vifaa wawapo shuleni," alisema Dk. Bakari.

Vilevile Dk. Bakari alimuomba Njeza awe mlezi wa kikundi hicho ili washirikiane kwenye malezi pamoja na kuwasaidia watoto hao kufikisha mahitaji yao serikalini ombi ambalo Njeza aliridhia.

Hata hivyo, baadhi ya watoto hao walisema wanakabiliwa na tatizo la unyanyapaa kuanzia kwenye familia, shuleni na mitaani kwa maelezo kuwa huwa wanatengwa na wenzao wanaojua kuwa wanaishi na maambukizi.



Mbunge wa Jimbo la Mbeya Vijijini, Oran Njeza (kushoto) akiwakabidhi wasimamizi wa kituo cha kutolea huduma kwa watoto wanaoishi na maambukizi ya Virusi vya Ukimwi (VVU) kilichopo katika Hospitali Teule ya Wilaya ya Ifisi alipojumuika na watoto hao mwishoni mwa wiki kusherehekea Sikukuu ya Krismasi. **PICHA NA NEBART MSOKWA**

# Wakulima waomba kujengewa soko maalumu la ndizi

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WAKULIMA wa ndizi katika Halmashauri ya Busokelo wilayani Rungwe, wameiomba serikali kuwajengea masoko maalumu ya zao hilo ili kupunguza tatizo la wakulima kuuzia mazao yao mashambani na kupunjwa.

Wakizungumza na Nipashe wakulima hao walisema kukosekana kwa masoko maalumu kunawafanya baadhi ya walanguzi kuendeleza mfumo wa kuchumbia ndizi zikiwa changa mashambani mfumo ambao ni wa unyonyaji.

Mmoja wa wakulima hao, Samwel Mwakanyamale alisema, ukosefu wa soko la uhakika la ndizi unasababisha bei kuwa ya chini ikilinganishwa na maeneo mengine yanayouza ikiwamo Kyela na Tukuyu.

Alisema katika eneo hilo mkungu wa ndizi ambao maeneo mengine unauzwa kwa Sh. 5,000, wao wanauza kati ya Sh. 2,000 na 3,000 kutokana na wanunuzi kusingizia gharama za usafirishaji.

"Unaweza ukapita kwenye shamba la mkulima ukaona mikungu mingi imekomaa ukadhani huyo mtu ni tajiri, lakini ukifuatilia unakuta wanasema alishakula pesa siku nyingi imebaki tu kuvuna, kwahiyo unakuta tunahudumia ndizi za wafanyabiashara," alisema Mwakanyamale.

Hivi karibuni wakati wa ziara ya viongozi wa Serikali ya Malawi mkoani Mbeya, Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera, aliwaagiza viongozi wa wilaya ya Rungwe kujenga vituo vya kuuzia ndizi ili kuwarahisishia wanunuzi pamoja na kuongeza thamani ya zao hilo.

Homera alitoa agizo hilo kutokana na ombi la viongozi wa Malawi ambao walitaka vituo hivyo vijengwe ili kuwarahishishia upatikanaji wa bidhaa hiyo pamoja na zingine.

# Serikali yasitisha vibali vya uchomaji moto mashamba

**Na Nebart Msokwa,** MAKETE

HALMASHAURI ya wilaya ya Makete mkoani Njombe imesitisha utoaji wa vibali vya moto kwa wakulima wanapoandaa mashamba kutokana na ongezeko la matukio ya kuunguza mashamba ya miti na kuwatia wawekezaji hasara.

Uamuzi huo ulitolewa mwishoni mwa wiki na Kaimu Mkurugenzi wa Halmashauri hiyo, Upendo Mgaya, wakati wa utoaji wa hati za kimila za umiliki wa ardhi kwa wananchi wa kijiji cha Ibaga kilichopo kata ya Mang'oto wilayani humo.

Mradi huo unafadhiliwa na shirika lisilokuwa la kiserikali la Panda Miti Kibiashara ambalo linafanya kazi ya kuhamasisha utunzaji wa mazingira katika maeneo mbalimbali ya mikoa ya Njombe na Iringa.

Upendo alisema matukio ya moto yamekuwa yakitokea mara kwa mara na kusababisha uharibifu wa mazingira pamoja na kuharibu uchumi wa watu kwa kuharibu miti ya wananchi.

Alisema, halmashauri hiyo imeamua kuzuia vibali vyote vya uchomaji moto kwenye mashamba na kwamba wakulima wanatakiwa kufukia nyasi wakati wa kulima badala ya kuchoma moto.

"Tulikuwa tunatoa vibali vya watu kuchoma moto kwenye mashamba yao, lakini sasa hivi tumesitisha kwa sababu moto umekuwa ukileta athari kubwa sana, kipindi cha kiangazi mwaka huu yametokea matukio mengi ya moto ambayo yametoa athari kubwa," alisema Upendo.

Alisema moto huo ulikuwa ukitokea viongozi wa serikali ya wilaya hiyo walikuwa wanashirikiana na wananchi kuudhibiti ili kupunguza madhara.

Mwakilishi wa Shirika la Panda Miti Kibiashara, Andrew Ferdinand alisema lengo la kutoa hati hizo za kimila kwa wananchi ni kuwasaidia kuweka usalama wa mashamba yao na kuepusha migogoro ya ardhi miongopni mwao.

Alisema pia wanatoa elimu ya upandaji wa miti kibiashara kwa wananchi pamoja na kuwafundisha njia za pamoja za kuzuia moto kwenye mashamba yao.

Ferdinand alisema wanawafundisha wananchi kutengeneza njia za pamoja za kuzuia moto kwenye mashamba yao ya miti ili kuepusha madhara makubwa.

"Lakini tunatumia njia ya matumizi bora ya ardhi kuwahamasisha wananchi kutenga maeneo maalumu kwa ajili ya kupanda miti, maeneo ya kilimo, malisho na makazi ili kuepusha shughuli hizi kuingiliana," alisema Ferdinand.

Diwani wa kata ya Mang'oto, Osmund Idawa, alisema hati ambazo wananchi walipatiwa zitasaidia kupunguza migogoro ya ardhi inayoibuka mara kwa mara hasa ya wananchi kugombea mipaka.

Alisema katika eneo hilo kulikuwa na migogoro kati ya kijiji na kijiji, mkulima na mkulima pamoja na taasisi na wananchi na kwa sasa hizo hati zitakuwa suluhisho.



## Polisi utalii na diplomasia kuimarisha usalama wa wageni

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

KATIKA kukabiliana na vitendo vya uhalifu Zanzibar, Wizara ya Utalii na Mambo ya kale imeanzisha polisi utalii na diplomasia kwa lengo la kuimarisha hali ya mazingira ya ulinzi na usalama kwa wageni mbalimbali wanaoingia nchini.

Akikabidhi askari 69 wa vikosi mbalimbali kwa Mkuu wa Mkoa wa Kusini Unguja, Rashid Hadidi Rashid, Katibu Mkuu wa wizara hiyo, Fatma Mabruuk, alisema utalii katika nchi ni shughuli muhimu za kuleta maendeleo ya uchumi na kwamba kikosi hicho kitasaidia kuondoa changamoto mbalimbali zinazojitokeza ndani ya nchi.

Alisema wizara imehakikisha wageni wanaoingia nchini wanarudi wakiwa katika hali ya usalama zaidi.

Kwa upande wake Mkuu wa mkoa huo amekitaka kikosi hicho kuwa wazalendo katika kupambana na vitendo vya kihalifu kwa wageni wanaoingia nchini na serikali haitomvumilia mtendaji yeyote atakayekwenda kinyume na maagizo yaliyopangwa.

Vile vile, aliwataka wananchi wa mkoa huo kutoa ushirikiano kwa kikosi hicho hasa wanapoona viashiria vya uvunjifu wa amani katika fukwe za bahari na watalii kupenda kutembelea.

Naye Mkuu wa Polisi utalii na diplomasia Zanzibar Ngeradius Kakoki, alisema kuwa lengo la kuazishwa kwa kikosi hicho ni kuhakikisha watalii wanaoingia na kutoka wako salama wao na mali zao.

Alisema watafanya kazi kwa kuzingatia sheria na miongozo ya nchi kwa kuwa ikiwa salama watalii watafika kwa wingi na serikali itazidi kupata mapato.

# ‘Matapeli waliza wengi wizi wa fedha kimtandao’

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

KAMISHNA Msaidizi wa Jeshi la Polisi Zanzibar (ACP) na Naibu Mpelelezi wa Makosa ya Jinai (DCI), Zuberi Seif Chembera, amesema wananchi kutokuwa na elimu ya kimtandao inawaathiri kuibiwa fedha zao kupitia mitandaoni.

Akizungumza na Nipashe jana ofisini kwake Makao Makuu ya Jeshi la Polisi Kilimani, alisema kutokana na ugeni wa matumizi ya mitandao matapeli wamekuwa wakitumia nafasi hiyo kwa kuwatapeli wananchi aidha kwa kuwapigia simu au kuwatumia ujumbe kuwa watume pesa kupitia simu ya mkononi kwa namba ambazo huwaelekeza.

Alisema Jeshi la Polisi jukumu lake kubwa ni kusimamia sheria na kuhakikisha inatekelezwa ili atakayekwenda kinyume achukuliwe hatua za kisheria.

Alisema Tanzania inatumia Sheria ya makosa ya kimtandao ya mwaka 2015 na baadhi ya matukio ya kimtandao yameainishwa kuwa ni makosa ya jinai.

Hata hivyo, alisema kuwa Zanzibar haina matukio makubwa ya wizi wa kimtandao, lakini imekuwa na matukio mengi ya kawaida ambayo hutokana na matumizi ya simu na vyombo vya kielektroniki.

“Mfano kuna matukio mengi ya wizi wa kimtandao ambayo unatumiwa ujumbe wa simu kuwa tuma pesa kwa namba hii na kwa sababu wananchi wengi hawana elimu wanaibiwa sana kwa kutuma pesa kupitia simu,” alisema.

Alisema matukio mengine mabaya ya kimtandao ni ya kijamii ikiwamo vitisho ambayo wananchi huyaripoti vituo vya polisi.

Kamishna huyo alisema Jeshi la Polisi katika kushughulikia kesi hizo wanakabiliana na changamoto ya kisheria kwa sababu hawana uwezo wa kupata maelezo ya mawasiliano ya moja kwa moja kutoka katika kampuni za simu mpaka waandike barua kuomba kampuni hizo kupatiwa taarifa.

“Sisi kama polisi hatuna uwezo wa kisheria kupata taarifa za mawasiliano kutoka katika kampuni za simu, sasa ikitokea mtu ameibiwa au ametishiwa maisha kwa kutumia simu hatuna uwezo wa kuona mpaka tuandike barua kwa kampuni ya simu watuletee ushahidi wa taarifa hizo,” alisema.

Pia, alisema kumekuwa na uchelewaji wa kupata taarifa kutoka kwa kampuni za mawasiliano ya simu na inafika wakati wananchi wanakata tamaa na kulitupia lawama Jeshi la Polisi kuwa linachelewa kufanya upelelezi na haki kutopatikana.

DCI Chembera alisema kuwa, kuna haja ya kuwapo kwa marekebisho ya Sheria ya Makosa ya Jinai ili Jeshi la Polisi linapotaka kufanya upelelezi wa kesi za makosa ya kimtandao liwe na uwezo wa kuona mawasiliano yaliyotumika katika kampuni za simu dhidi ya malalamiko yaliyowasilishwa vituoni.

“Ushauri wangu serikali ione umuhimu wa kufanya marekebisho ya sheria na kama polisi tumeaminiwa kwenye mambo mengi makubwa na kwa hili watuamini tuwe na vifaa tuweze kupata taarifa za wizi wa mitandao ili kesi hizi kwenda kwa haraka zaidi,” alisema.

Kadhalika aliwataka wananchi kutotuma fedha kwa mtu ambaye hawamfahamu wala kujibu ujumbe wa simu wowote atao-tumiwa na mtu asiyemfahamu kuhusu muamala wa fedha.

Aliwataka watumiaji wa simu za mkononi kuwa makini kwenye matumizi kwa sababu ni kama silaha yaweza ikamjeruhi yeye mwenyewe au kumjeruhi mtu mwengine endapo hataitumia vizuri.

Naye Mkurugenzi wa Taassi ya kusaidia vijana (Zanzibar Youth Foram), Maulid Suleiman, alisema taasisi hiyo imekuwa ikitoa elimu kwa vijana kuhusu matumizi sahihi ya kimitandao na vijana ndiyo kundi kubwa la watumiaji.

Aliwataka vijana kutokuwa na tamaa ya kutaka kupata fedha kwa haraka na baadhi yao kujihusisha na wizi wa kimtandao.



Waziri wa Fedha na Mipango Jamal Kassim (Wapili kulia) akizungumza katika kikao cha pamoja cha kujadili changamoto za kiwanda cha Sukari Mahonda akiwa na baadhi ya mawaziri, Waziri wa Kilimo, Dk Soud Nahoda (kulia), Waziri wa Ardhi Riziki Pembe (kushoto), Waziri wa Uwekezaji Mudrik Soraga na Waziri wa Biashara na Viwanda, Omar Said. **PICHA: RAHMA SULEIMAN.**

## Muswada kuundwa mamlaka kamili kudhibiti madawa kulevya wapitishwa

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAJUMBE wa Baraza la Wawakilishi wamepitisha muswada wa kisheria wa kuundwa kwa mamlaka kamili ya kudhibiti na kupambana na madawa ya kulevya ambayo itakuwa na uwezo wa kukamata, kufanya upelelezi pamoja na kufikisha mahakamani watuhumiwa.

Mswada huo umepitishwa katika kikao cha Baraza la Wawakilishi baada ya kuwapo kwa mchuano mkali wa ufafanuzi wa tafsiri za vifungu vya muswada huo na kazi ya ufafanuzi ikifanywa na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais, Dk. Sada Mkuya, pamoja na Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Dk. Mwinyi Talib Haji.

Muswada huo utajumuisha matumizi ya bangi na mengine kutambuliwa kuwa ni sehemu ya dawa za kulevya na atakayekamatwa na kutiwa hatiani adhabu yake ni kifungo cha maisha jela.

Waziri Mkuya alisema serikali imelazimika kufanya marekebisho ya kuja na sheria ya kuundwa kwa mamlaka ya kudhibiti na kupambana na dawa za kulevya baada ya sheria iliyokuwapo awali kushindwa kufanya kazi vizuri na kuleta mafanikio.

Alisema Sheria ya Tume ya kudhibiti na kuratibu dawa za kulevya haikuwa na uwezo wa kukamata, kufanya uchunguzi na kufikisha mahakamani kazi ambayo hufanywa na Jeshi la Polisi na kuacha shaka na maswali.

“Kupitishwa kwa sheria ya kuundwa kwa mamlaka kamili ya kupambana na madawa ya kulevya sasa tumeandika historia mpya kwamba tupo tayari kutokomeza madawa ya kulevya,” alisema.

Baadhi ya wajumbe wa Baraza hilo waliochangia muswada huo walisema ni sheria nzuri yenye nia ya dhati ya kupambana kikamilifu na madawa ya kulevya pamoja na athari zake kwa ujumla.

Waziri wa Biashara na Maendeleo ya viwanda, Omar Said Shaaban, alisema sheria hiyo itaijengea Zanzibar heshima na matumaini makubwa mbele ya wawekezaji katika kupambana na dawa za kulevya na kuitambulisha Zanzibar kuwa ipo salama.

Mwakilishi wa Jimbo la Mfenesini, Machano Othman Said, aliitaka mamlaka ya kupambana na madawa kulevya kuendelea kushirikiana na Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP), yenye uzoefu wa kuendesha kesi mbalimbali za jinai.

“Naunga mkono ingawa naiomba mamlaka ya kupambana na madawa ya kulevya kuendelea kujenga mashirikiano na Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP) katika kusaidiana na kusimamia kesi za jinai,” alisema.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KIWANJA KIANUZWA.

KIWANJA KIANUZWA KISUSURU JKT KIWANJA KIPO KISUSURU JKT SEGEREA UKUBWA SQM 2252 KINA HATI BEI MILIONI 55, **KWA MAWASILIANO: 0786 857523 AU 0655 857523**

## KIWANJA KIANUZWA.

KIPO MINGOI MPAKANI MWA BUJU NA MAPINGA.NDANI KUNA PAGALE LA KUPAUA NA MSINGI WA VYUMBA NA SEBULE.BARABARA ,MAJI VIPO KIMEPIMWA

BEI NI TSHS.MILIONI KUMI (10,000,000/=)TU

**MAWASILIANO:0782 574 669 AU 0621 879 477**

OFISI ZA MATANGAZO MIKOCHENI INDUSTIAL AREA, PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.
MOB: +255 - 0782253676

## KUPOTEA KWA CHETI



**NSHOMA MASULE NTEBA** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **P2517-0500** kilichotolewa na baraza la mitihani kupitia kituo/shule ya **ALFA SECONDARY CENTRE** mwaka **2019**, yeyote atakayekiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi
Polisi taarifa **MOR/MOR/RB/259264/2021**

**IN THE HIGH COURT OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**IRINGA DISTRICT REGISTRY**
**AT IRINGA**
**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO.1 OF 2021**
**IN THE MATTER OF THE ESTATE OF THE LATE KENNETH ELLY NYANGOYA**
**AND**
**IN THE MATTER OF AN APPLICATION FOR LETTERS OF ADMINISTRATION BY SALOME DAUDI WERE AND OTIENO ELLY NYANGOYA**

**NOTICE TO CREDITORS**

**NOTICE** is hereby given that all persons claiming debts or liabilities affecting the estate of the above named **KENNETH ELLY NYANGOYA** deceased, who died at dar es salaam on the 13th day of October 2019 and letters of administration of whose estate were granted to us by the court on the 09th November 2021 are hereby required to send in their claims to us at the following address p.o.box 19708 **DAR ES SALAAM** within 60 days from the date of the publication of this notice at the expiration of which shall proceed to hand over assets to the persons entitled thereto having regard only to the claims of which we shall then have had notice.

**SALOME DAUDI WERE** (administratrix)
**OTIENO ELLY NYANGOYA** (administartrix)

**IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA**
**AT DODOMA**
**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO…………………….. 2021**
**In the Matter of the Estate of the late AGNES LITUS CHARLES of MAILI MBILI within Dodoma Region.**
**AND**
**IN THE MATTER OF THE APPLICATION FOR LETTERS OF ADMINISTRATION BY CHARLES LITUS KAMOGA**
**GENERAL CITATION**
**(RULE 75 of PROBATE RULES GN 369 of 163)**

All PERSONS claiming to have any interest in the Estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named Petitioner.
Objections to the grant should be filed on or before 17/01/2022.
Dated at Dodoma this……………..Day of…………………………2021
Presented for filing this…………………day of…………………..2021

RESIDENT MAGISTRATE

**HALMASHAURI YA MANISPAA YA- ILEMELA**
**BARUA ZOTE ZIANDIKWE KWA MKURUGENZI WA MANISPAA**

**Kumb Na. IMC/L/802/35/FDM**
**Kwa yeyote anayehusika,**
**SHERIA YA USAJILI WA ARDHI (SURA 334)**
**KUPOTEA KWA BARUA YA TOLEO PAMOJA NA STAKABADHI ZA MALIPO YA KIWANJA**

Barua ya Toleo (letter of offer) ya kiwanja pamoja na stakabadhi za malipo ya kodi ya kiwanja (new offer charges &land rent receipts),kiwanja Na.244 Kitalu 'F' Nyamanoro.

Mmiliki aliyeandikishwa: EVARIST MUSHI wa S.L.P 1953, Mwanza.
Muombaji: MADLASTA SHAYO SIFUEL wa S.L.P 1935,Mwanza.
Ardhi: kiwanja Na.244 Kitalu 'F' Nyamanoro,Manispaa ya Ilemela.
TAARIFA IMETOLEWA Kwamba Barua ya Toleo ( Letter of offer) ya kiwanja pamoja na stakabadhi za malipo ya kodi ya kiwanja ya kumiliki ardhi (New offer charges &land rent receipts) vilivyotajwa hapo juu vimepotea na ninakusudia kutoa Nakala halisi ya Barua ya toleo (letter of offer) ya kiwanja badala yake iwapo hakuna kipingamizi chochote kwa muda wa mwezi mmoja tokea tarehe ya taarifa hii.

Barua ya Toleo(letter of offer) ya kiwanja pamoja na stakabadhi za malipo ya kodi ya kiwanja (New offer charges & land rent receipts) halisi vikionekana virudishwe Manispaa ya Ilemela, S.L.P 735,Mwanza.

**Fredrick D.Michael**
**k.n.y. MKURUGENZI WA MANISPAA**
**ILEMELA**

Fredrick D.Michael
**k.n.y. MKURUGENZI WA MANISPAA**
**ILEMELA**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA.**
**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA LA WILAYA**
**KAGERA LILILOPO BUKOBA**
**MAOMBI MADOGO NA: 65/ 2021.**
**WILLIAM NDEGE NDYETABULA………………MWOMBAJI**
**DHIDI YA**
**SHABAN GERASE………………………………… MJIBU MAOMBI**
**KWA: SHABAN GERASE**
**(POPOTE PALE ULIPO)**

Unaarifiwa kuwa Maombi madogo Na. 65/2021 yamepangwa kutajwa tarehe 31/01/2022 mbele ya Mwenyekiti wa Baraza, R.Mtei saa2:00 Asubuhi.
Hivyo, unaamuriwa kuhudhuria wewe mwenyewe/ mwakilishi wako mbele ya Baraza siku hiyo bila kukosa. Usipohudhuria Baraza litasikiliza shauri upande mmoja dhidi yako na hukumu kutolewa.
AMRI. Hii imetolewa kwa mkono wangu na MUHURI wa Baraza hili leo tarehe 07/11/2021.

…………………………
**MWENYEKITI**
**BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA**
**BUKOBA.**

**BITCHANGE COMPANY LIMITED**
**P O BOX 38604 DAR ES SALAAM TANZANIA**
**EXTRACTED SPECIAL RESOLUTION FROM THE MINUTES OF THE BOARD MEETING OF BITCHANGE COMPANY LIMITED ON THE 02 JANUARY 2021**
**AT ILALA KARIAKOO, AGREY**

At the above named meeting of the board of directors of Bitchange Company Limited the said board of directors,

On the issue of voluntary winding up of the company,Bitchange company limited

Resolved that due to the members shareholders loss of internet to continue doing business and by reason of cost operation business is very high than the profit obtained, that is Bitchange company limited, the they said company should be voluntary wound up according to the procedure laid down by the law in Tanzania

Resolved that Suma David Malekela and Leonard David Malekela were thereby appointed to be the liquidator of the company,tha is Bitchange company limited to the law of Tanzania

**Extracted this 02nd of January 2021**

**BITCHANGE COMPANY LIMITED**
**COMPANY NUMBER 138588**
**BUSINESS REGISTRATION AND LICENSING AGENCY**
**NOTICE OF WIND UP OF A COMPANY**

NOTICE IS HEREBY GIVEN to the general public, that according to the section 334(1)of the companies act no.12 of 2002,member of the company was provided a notice of call to winding up company which held at dar es salaam,ilala dated 27/04/2021 have voluntary decided to wind up the company.

*Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie 0782253676*

NJOO UTANGAZE BIDHAA YAKO KWA BEI NAFUU SANA

Kwa Habari Motomoto
usikose Gazeti lako
la Nipashe kila siku
Tupigie
0782253676
Nipashe
MWANGA WA JAMII

OFISI ZA MATANGAZO
MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,
PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.
E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

HABARI KIMATAIFA

# Papa Francis, Malkia, Biden wamuombolezea Desmond Tutu

## • Mazishi kitaifa Jan. Mosi 2022

Na Christina Mwakangale

UBAGUZI wa rangi ni kati ya masuala makuu yaliyoitikisa Afrika Kusini, ilichukua miongo kadhaa kuondoka nchini humo, wamo viongozi mashuhuri waliopigana kuhakikisha kuna usawa, akiwamo Askofu Desmond Tutu, hadi kutuzwa Tuzo ya Nobel, kutokana na harakati hizo.

Kifo cha Askofu Tutu kilitangazwa juzi, nchini Afrika Kusini, akifariki akiwa na miaka 90, kinafanya Waafrika Kusini Waafrika, Dunia kwa ujumla kumkumbuka, kutokana na kupinga ubaguzi wa rangi.

Rais wa Afrika Kusini, Cyril Ramaphosa ametangaza bendera zitapepea nusu mlingoti nchi nzima pia katika balozi za Afrika Kusini nje ya nchi, hadi usiku wa kuamkia ibada ya mazishi.

Mipango ya mazishi inaendelea na kwa siku mbili, mwili wake utawekwa mahali maalumu ili kutazamwa kabla ya mazishi rasmi ya serikali, Januari Mosi, 2022, mjini Cape Town.

Kengele za Kanisa Kuu la St George, zitalia kwa dakika 10 kila siku saa sita mchana hadi siku ya Ijumaa kwa heshima ya shujaa wa kupinga ubaguzi wa rangi, Afrika Kusini.

Risala zimekuwa zikimiminika kutoka kwa viongozi kote duniani, akiwamo Papa Francis, Rais wa Marekani, Joe Biden na Malkia Elizabeth II wa Uingereza.

Tangu kutangazwa kwa kifo chake, Jumapili, maelfu ya Waafrika Kusini wamekuwa wakijitokeza kwenye Kanisa Kuu la St. George, kutoa salamu za heshima na rambirambi kwa Askofu Tutu.

Wengi wanaweka mashada ya maua chini ya picha ya askofu, iliyopo mbele ya jengo hilo la kanisa la kale mjini Cape Town.

Rais wa Afrika Kusini Cyril Ramaphosa alisema katika taarifa yake kwamba Tutu amesaidia kuleta "Afrika Kusini iliyokombolewa".

Tutu aliyeishi wakati wa Nelson Mandela, alitunukiwa tuzo ya Nobel mwaka 1984 kwa mchango wake katika mapambano ya kukomesha mfumo wa ubaguzi wa rangi uliotekelezwa na serikali ya wazungu wachache dhidi ya weusi walio wengi nchini Afrika Kusini kuanzia 1948 hadi 1991.

Kifo cha Tutu kimekuja ikiwa ni wiki chache tu baada ya kile cha rais wa mwisho wa enzi ya ubaguzi wa rangi wa Afrika Kusini, FW de Klerk, aliyefariki akiwa na umri wa miaka 85.

"Umuhimu wake unavuka mipaka ya kuwa Mwanglikana," muombolezaji Brent Goliath aliambia shirika la habari la AFP, akiangua kilio.

"Nilihamaki sana asubuhi ya leo niliposikia kwamba alikuwa ameaga dunia. Ninamshukuru Mungu kwa kuwa amekuwa kwa ajili yetu," Goliath alisema, akiongeza kwamba alikutana na Tutu mara kadhaa.

### RAMBIRAMBI DUNIANI

Viongozi kutoka kote duniani wametoa risala zao, akiwamo

Rais Biden akisema "alivunjika moyo kufahamu kuhusu kufariki kwa mtumishi wa kweli wa Mungu na watu", akiongeza kuwa "urithi wa Tutu unavuka mipaka na utaendelea kwa muda mrefu".

Rais wa zamani wa Marekani, Barack Obama, alimtaja Tutu kama "mshauri, rafiki na dira ya maadili".




Mwaka 2013, Rais wa wakati huo wa Marekani, Barack Obama, akiwa na Askofu Desmond Tutu mara baada ya kutembelea Wakfu wa Vijana wa Desmond Tutu, kuhusu HIV huko Cape Town nchini Afrika Kusini.



Askofu Mkuu Desmond Tutu akiwa na Malkia wa Uingereza, Elizabeth II mjini Cape Town mwaka 1995. **PICHA ZOTE: BBC**

Katika ujumbe wa rambirambi, Malkia Elizabeth II alisema alikumbuka kwa furaha mikutano yake na yeye, na uchangamfu wake mkubwa na ucheshi.

"Kuaga dunia kwa Askofu Mkuu Tutu kutahisiwa na watu wa Afrika Kusini na watu wengi huko Uingereza, Ireland ya Kaskazini na katika Jumuiya ya Madola, ambapo alishikiliwa kwa upendo na heshima kubwa."

Vatican, ilisema katika taarifa kwamba Papa Francis alitoa rambirambi za moyoni kwa familia yake na wapendwa wake.

"Akizingatia huduma yake kwa injili kupitia kukuza usawa wa rangi na upatanisho katika nchi yake ya asili ya Afrika Kusini, utakatifu wake unaipongeza roho yake kwa huruma ya upendo ya Mwenyezi Mungu."

"Kupigania uhuru kutoka kwa mahandaki ya Afrika Kusini kulihitaji ujasiri ambao hauwezi kuelezeka," Graca Machel, mjane wa Nelson Mandela, alisema katika taarifa yake.

Pia, Wakfu wa Nelson Mandela ulikuwa miongoni mwa waliotoa risala, ukisema michango ya Tutu katika mapambano dhidi ya dhuluma, ndani na nje ya nchi, inalingana tu na kina cha mawazo yake kuhusu kutengeneza mustakabali wa ukombozi kwa jamii za wanadamu".

"Alikuwa binadamu wa ajabu. Mwanafikra. Kiongozi. Mchungaji."

### VAZI LILILOMTAMBULISHA

Alijulikana kwa upendo kama The Arch, Tutu alitambulika papo hapo, akiwa na mavazi yake ya zambarau ya ukasisi, hali ya uchangamfu na tabasamu karibu kila mara.

Hakuogopa kuonyesha hisia zake hadharani, ikiwa ni pamoja na kucheka na kucheza kwa kumbukumbu katika sherehe za ufunguzi wa Kombe la Dunia la Kandanda Afrika Kusini mwaka 2010.

Licha ya umaarufu wake, hata hivyo, hakuwa mtu ambaye alipendwa na wote.

Aliikosoa sana serikali ya African National Congress (ANC) katika enzi ya baada ya ubaguzi wa rangi, wakati fulani, alihisi kuwa inawakilisha vibaya Afrika Kusini, hata kuonya mwaka 2011 kwamba angeiombea kuanguka kwa ajili ya kufutwa kwa ziara ya Dalai Lama.

Alitawazwa kama kuhani mwaka wa 1960, Tutu aliendelea kuhudumu kama askofu wa Lesotho kuanzia 1976 hadi 1978, askofu msaidizi wa Johannesburg na mkuu wa parokia, Soweto.

Alikuwa Askofu wa Johannesburg mwaka 1985 na aliteuliwa kuwa Askofu Mkuu wa kwanza mweusi wa Cape Town mwaka uliofuata. Alitumia nafasi yake ya hadhi ya juu kuzungumzia ukandamizaji dhidi ya watu weusi nchini mwake, siku zote akisema nia yake ni ya kidini na si ya kisiasa.

Baada ya Mandela kuwa rais wa kwanza mweusi wa Afrika Kusini mwaka 1994, Tutu aliteuliwa naye kwenye Tume ya Ukweli na Maridhiano iliyoundwa kuchunguza uhalifu uliofanywa na wazungu na weusi wakati wa enzi ya ubaguzi wa rangi.

Pia alisifiwa kwa kubuni neno Rainbow Nation, kuelezea mchanganyiko wa makabila ya Afrika Kusini baada ya ubaguzi wa rangi, ingawa katika miaka yake ya mwisho alielezea masikitiko yake kwamba taifa hilo halijaungana kwa namna ambayo alikuwa na ndoto.

### MAZISHI

Dayosisi ya Pretoria na Baraza la Makanisa la Afrika Kusini, watafanya ibada ya kumbukumbu katika mji mkuu, kesho.

Keshokutwa jioni, Askofu Mkuu wa Tutu IP Trust na Desmond & Leah Tutu Legacy Foundation, wataandaa hafla kwa marafiki wa Watutu, taarifa yao ilisema.

Siku ya Ijumaa, Askofu Mkuu Tutu atalala katika Jimbo la St George, kabla ya ibada ya mazishi Jumamosi itakayoongozwa na Askofu Mkuu Makgoba.

"Tunatoa shukrani zetu za dhati kwa watu na mashirika kote nchini na duniani kote kwa kumiminiwa upendo, heshima na rambirambi kufuatia kifo cha Askofu," Askofu Mkuu Tutu IP Trust na Wakfu wa urithi wa Desmond & Leah Tutu walisema katika taarifa yao. **MTANDAO**

HABARI MICHEZO

# BARAZA AITAKA KAGERA SUGAR 'KUVUNJA BENKI' ISAJILI STRAIKA

Na Saada Akida

KOCHA Mkuu wa Kagera Sugar, Francis Baraza, amesema iwapo viongozi wa timu hiyo wakikubali 'kuvunja benki' (kutoa kiasi kikubwa cha fedha) ili kuimarisha kikosi chao, eneo ambalo atalimulika zaidi ni nafasi ya ushambuliaji kwa kusajili nyota wawili kuelekea michezo yao ya Ligi Kuu Tanzania Bara.

**Akizungumza na gazeti hili jijini Dar es Salaam jana, Baraza alisema hawako katika nafasi nzuri na ameona mapungufu ya kikosi chake yapo zaidi kwenye safu ya ushambuliaji, hivyo anatakiwa kuongeza nyota wawili.**

Alisema endapo viongozi watashindwa kutoa kiasi kikubwa cha fedha ambazo zitamwezesha kupata washambuliaji wawili wenye uzoefu mkubwa, basi atahitaji straika mmoja na kiungo mkabaji.

"Nimeangalia kwa hizi mechi 10 tulizocheza nimeona jinsi vijana wangu wanapambana kwa kutengeneza nafasi nyingi, lakini tumekosa mtu wa kumalizia, sasa nahitaji mshambuliaji mwenye uzoefu na utulivu.

"Iwapo viongozi watakubali kuvunja benki, basi nitasajili washambuliaji wawili kama hakutakuwa na fedha, nitalazimika kusajili straika mmoja na kiungo mkabaji mmoja," alisema Baraza.

Alisema kwa washambuliaji anaangalia zaidi nje ya nchi kutokana na misimu miwili iliyopita kwa wazawa ni John Bocco (Simba) na Adam Adam ndio wamekuwa na mwendelezo mzuri wa kupambana na wachezaji wa kigeni.

"Ukiachana na majina hayo ya wazawa, yaliyobakia ni wachezaji wakigeni ndio wanazidi kusumbua, hivyo licha ya kutaka kuwaboresha hawa niliokuwa nao, lakini nahitaji watu wakuja kuleta ushindani na kupambania timu kufikia malengo," alisema Baraza.

Alisema kwa sasa wako katika nafasi mbaya katika msimamo na wanapigania ndani ya mzunguko wa kwanza kujikwamua kutoka chini na kupanda juu ya msimamo.

Kagera Sugar wako nafasi ya 13 baada ya kushuka dimbani mara 10 na kujikusanyia alama tisa pekee kutokana na kushinda mechi tatu na kupoteza saba.

POLENI SANA...



Rais Mstaafu, Dk. Jakaya Mrisho Kikwete (Kushoto), akiteta jambo na Bondia Hassan Mwakinyo baada ya kuwasili nyumbani kwao jijini Tanga jana kwa ajili ya kutoa pole kwa familia ya bondia huyo kwa kufiwa na mama yake mzazi, Fatuma Hassan Siri. Kulia ni Mkuu wa Mkoa wa Tanga, Adam Malima. **NA MPIGAPICHA WETU**

# *Metacha yupo kambini - Polisi Tanzania*

Na Adam Fungamwango

KLABU ya Polisi Tanzania, imeshangazwa na uvumi unaomhusisha golikipa wake namba moja Metacha Mnata kuwa amevunja mkataba na timu hiyo akiwa katika harakati za kurejea klabu ya Yanga, ikidai kipa huyo bado ni mali yao na yupo kambini akijiandaa na mechi ya Ligi Kuu.

Mratibu wa klabu hiyo, Ramadhani Tamim, amesema mpaka sasa wao kama uongozi hawajapata taarifa yoyote ya Yanga kumtaka kipa huyo au kuvunja mkataba kama inavyodaiwa.

"Na sisi tunazisikia na tunazisoma taarifa hizo kama ninyi, sijui zinaanzia wapi, lakini mpaka sasa hatujapata taarifa yoyote kuhusiana na kipa wetu kuvunja mkataba au klabu inayomtaka kuja kuzungumza na sisi. Tuna utaratibu wa kusajili ambao mchezaji tukitaka kumsainisha tunampeleka kwa mwanasheria wetu, na hata kama anataka kuvunja mkataba ni lazima kwanza lifike kwa mwanasheria wetu, lakini hilo mpaka sasa halijafanyika na hivi ninavyokwambia mchezaji yupo kambini na wenzake akijiandaa na mechi ya ligi, ila kama huko mbele likitokea lolote lile tutasema, lakini kwa sasa hatuna taarifa yoyote," alisema Tamim.

Jana, Polisi Tanzania ilitarajiwa kucheza dhidi ya Mbeya City kwenye Uwanja wa Ushirika mjini Moshi.

Tetesi za usajili wa kipa huyo wa zamani wa Yanga, kurejea kwenye klabu hiyo zimeenea kwenye mitandao ya kijamii, akiandika maneno yanayoashiria kumuaga meneja wake Jemedari Said na kuonekana hawatokuwa wote tena kama mtu na meneja wake.

Klabu ya Yanga inadaiwa inasaka kipa, kutokana na Djigui Diarra kuwa sehemu ya kikosi cha timu ya Taifa ya Mali kitakachoshiriki fainali za Mataifa ya Afrika (AFCON), mwezi ujao nchini Cameroon.

Hata hivyo, Ofisa Habari wa Klabu ya Yanga, Hassan Bumbuli, naye ameibuka na kusema kuwa mpaka sasa mezani kwao hawana mpango wowote wa kumtwaa kipa huyo.

# KMC, Ruvu Shooting kujiuliza Ligi Kuu leo

Na Saada Akida

LIGI Kuu Tanzania Bara itaendelea leo kwa kupigwa mechi mbili kwa KMC FC kuwakaribisha Ruvu Shooting katika Uwanja wa Azam Complex, Chamazi nje kidogo ya Jiji la Dar es Salaam huku Coastal Union ikiwa mwenyeji wa Mtibwa Sugar kwenye dimba lao la Mkwakwani jijini Tanga.

KMC itashuka dimbani leo ikiwa na kumbukumbu ya kupoteza mechi iliyopita dhidi ya Simba katika Uwanja wa Ali Hassan Mwinyi mkoani Tabora wakati Ruvu Shooting walikubali kichapo kutoka kwa Azam FC katika Uwanja wa Chamazi.

Wakizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana, Kocha Msaidizi wa Ruvu Shooting, Mohammed Nakuchema, alisema wamejiandaa vizuri kwenda kupambana kutafuga matokeo mazuri katika mchezo huo.

Alisema wataendelea kuwakosa nyota wake 11 kati yao 10 wako katika mafunzo ya kijeshi, hivyo wamelazimika kufanya mabadiliko katika kikosi chao kulingana na wachezaji watakaowakosa katika mchezo huo.

"Kutokuwapo kwa nyota hao hakutaathiri mipango yetu kwa sababu nyota wengine wapo na wako fiti na tayari kwenda kupambana na KMC FC kutafuta matokeo chanya," alisema Nakuchema.

Naye Kocha Mkuu wa KMC FC, Habib Kondo (pichani), alisema



baada mchezo uliopita dhidi ya Simba, wamefanyia kazi mapungufu yao na kujiimarisha kuelekea mchezo wao wa leo dhidi ya Ruvu Shooting.

Alisema malengo yao makubwa ni kuhakikisha wanafanikiwa katika mechi tano za mzunguko wa kwanza kwa kupata matokeo ikiwemo huo wa leo.

Alisema kutokana na jinsi ligi ilivyokuwa na ushindani anaamini hata mchezo wa leo utakuwa mgumu kwa sababu kila mmoja wao anahitaji kupata matokeo chanya ili kujiweka katika mazingira mazuri kwenye msimamo.

"Ruvu Shooting ni wazuri tunahitaji kupata matokeo na kila mmoja amejianda vizuri, kwa upande wetu tumejiandaa kuhakikisha tunafanikiwa kupata matokeo," alisema Kondo.

## ZISIKUPITE

### BALE, ISCO KUONDOKA

MSHAMBULIAJI wa Wales, Gareth Bale mwenye umri wa miaka 32, na kiungo wa kati wa Hispania, Isco mwenye miaka 29, wataondoka Real Madrid Januari, huku mikataba ya wachezaji wote wawili zikimalizika msimu wa majira joto. ***(Marca)***

### REAL UHAKIKA KWA MBAPPE

REAL Madrid inazidi kuwa na uhakika wa kumsajili mshambuliaji wa Ufaransa, Kylian Mbappe kutoka Paris St-Germain, ingawa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 23, anaweza kusaini mkataba wa awali na klabu ya kigeni kuanzia Januari Mosi. ***(AS, via Mail)***

### TORRES RASMI BARCA

MSHAMBUIAJI wa Manchester City, Fernando Torres mwenye umri wa miaka 21, yuko nchini kwao Hispania na jana Jumatatu alifanyiwa vipimo vya afya kabla ya kukamilisha uhamisho wake wa kwenda Barcelona. ***(Mundo Deportivo)***

### WANNE KUTUA UNITED

MANCHESTER United inalenga wachezaji wanne wa Ujerumani inaotarajia kuwasajili. Kiungo wa kati wa Bayern Leverkusen, Florian Wirtz, 18, mlinzi wa kushoto wa Borussia Monchengladbach, Luca Netz, 18, kiungo wa kati wa RB Lepizig, Eric Martel na beki wa kati wa VFL Bochum Armel Bella-Kotchap, 20, wote ni miongoni mwa wanaolengwa na kocha wa muda, Ralf Rangnick. ***(Sun)***

### KAMARA ATAKIWA NEWCASTLE

NEWCASTLE United wanapanga kumsajili kiungo wa Marseille, Boubacar Kamara, 22. Mfaransa huyo ni mchezaji huru mwishoni mwa msimu huu, huku Manchester United na Chelsea pia zikivutiwa naye. ***(Sun)***

### MAITLAND-NILES KUTUA ROMA

KIUNGO wa kati wa England, Ainsley Maitland-Niles, 24, yuko tayari kuondoka Arsenal na kujiunga na AS Roma ya Italia kwa mkopo. ***(Goal)***

### RUDIGER SAFI MADRID

REAL Madrid wanatarajia mlinzi wa Chelsea na Ujerumani, Antonio Rudiger, 28, atajiunga nao bila malipo mwishoni mwa msimu huu. Huku ikiwa imesalia miezi sita pekee katika mkataba wake. ***(Telegraph)***


### MOYES AMTAKA KELLY

KOCHA wa West Ham, David Moyes ana nia ya kumsajili beki wa kati wa England, Lloyd Kelly, 23, kutoka Bournemouth. ***(Telegraph)***

### GALLAGHER KURUDI CHELSEA

KOCHA wa Chelsea, Thomas Tuchel amependekeza kiungo wa kati wa England, Conor Gallagher, 21, kurejea Stamford Bridge kupigania nafasi yake baada ya kumalizika kwa mkopo wa muda mrefu katika klabu ya Crystal Palace. ***(Metro)***

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# MARTIAL: SASA NATAKA KUONDOKA MAN UNITED

Lakini ameambiwa klabu haijapata ofa yoyote kutoka kwingineko na kwamba ikiwa hivi...

**MANCHESTER,** England

NYOTA wa Ufaransa, Anthony Martial, amemwambia kocha wa muda wa Manchester United, Ralf Rangnick anataka kuondoka.

**Rangnick alisema "alizungumza kwa kirefu" siku ya Jumatano na kijana huyo mwenye umri wa miaka 26, ambaye alimwambia "ni wakati muafaka wa mabadiliko".**

Martial ameanza mechi mbili pekee za Ligi Kuu England msimu huu, akifunga mara moja.

Licha ya kutaka kuondoka Old Trafford, Rangnick alithibitisha kuwa klabu hiyo bado haijapokea ofa ya kumnunua mshambualiaji huyo.

Wakala wa mchezaji huyo, Philippe Lamboley alithibitisha mapema mwezi huu Martial alitaka kuondoka katika klabu hiyo Januari, na kuongeza kuwa "atazungumza na klabu hivi karibuni".

Rangnick alisema: "Alinieleza kuwa amekuwa Manchester United sasa kwa miaka saba iliyopita na anahisi ni wakati muafaka wa mabadiliko, kwenda mahali pengine."

Martial alisajiliwa na United mwaka 2015 kutoka Monaco kwa pauni milioni 36 na kumfanya kuwa mwanasoka ghali zaidi duniani wakati huo.

Amefunga mabao 79 katika mechi 268 akiwa na 'Mashetani Wekundu' hao, lakini amekuwa hana nafasi baada ya kuwasili kwa Cristiano Ronaldo, Edinson Cavani na Jadon Sancho.

Hajashiriki katika mechi yoyote ya Rangnick kama kocha hadi sasa na amecheza mechi 10 pekee katika mashindano yote msimu huu.

"Nadhani kwa njia hii inaeleweka," aliongeza Rangnick.

"Ningeweza kufuata mawazo yake, lakini kwa upande mwingine, ni muhimu pia kuona hali ya klabu. Tuna nyakati za Covid, tuna mashindano matatu ambayo tuna matarajio makubwa na tunataka kuwa na mafanikio kadri tuwezavyo.

"Hadi sasa, nijuavyo, hakujawa na ofa yoyote kutoka kwa klabu nyingine yoyote na mradi iwe hivi atabaki."

MECHI KALI
HOME
AWAY
LEICESTER
6.61 | 5.41 | 1.38
LIVERPOOL

KUWEKA PESA:
- PIGA *150*87#,
CHAGUA 4
- WEKA PESA.
tigo pesa
vodacom m-pesa
halopesa
airtel money
ZANTEL EZYPESA
SEND

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#
GBT:0249
18+
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA:
0764115588, 0677115588
0685115588
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

CHEZA USHINDE KASINO



# TERRY AJIANDAA KURUDI CHELSEA

**LONDON,** England

MLINZI wa zamani wa klabu ya Chelsea, John Terry, anajiandaa kurudi tena kwenye klabu yake ya zamani baada ya miaka mitano kuchukua mikoba ya kuwa kocha wa timu ya vijana.

Terry mwenye umri wa miaka 41 aliachana na Chelsea na kutumia muda huo kufanya kazi za ukocha huku akitumia miaka mitatu kwenye klabu ya Aston Villa akiwa kama kocha msaidizi wa Dean Smith kabla ya kuondoka majira ya joto.

Nahodha huyo wa zamani wa timu ya Taifa ya England, baada ya kuachana na klabu ya Aston Villa, alizunguka nchi mbalimbali za Ulaya akijifunza aina tofauti ya mifumo ya ukocha na kusubiri kazi mpya.

Baada ya kuona wachezaji wenzie wa zamani kama Wayne Rooney, Frank Lampard na Steven Gerrard wakianza kufanya kazi zao kwa mara ya kwanza nje ya Ligi Kuu England, Terry naye anaamini anaweza kupitia njia hiyo pia.



# Mbappe azipasua kichwa PSG, Madrid

**PARIS,** Ufaransa

MSHAMBULIAJI wa klabu ya PSG, Kylian Mbappe hatima yake inaweza kuamuliwa baada ya mchezo wa Ligi ya Mabingwa Ulaya kati ya Paris Saint-Germain na Real Madrid mwakani.

Ingawa PSG imeandaa mkataba mrefu na wenye fedha nyingi ili kuweza kumbakisha kwenye dimba la Parc des Princes, lakini klabu ya Real Madrid ina matumaini makubwa kuwa wanaweza kumsajili akiwa huru, Mbappe anaweza kusaini mkataba wa awali na klabu yoyote kuanzia Januari Mosi.

Mbappe alishaweka wazi kuwa alikuwa anataka kuondoka kwenye dirisha la usajili la majira ya kiangazi ingawa ilishindikana, lakini klabu ya PSG bado ina matumaini kuwa inaweza kumbakisha mshambuliaji huyo kwa kumpa mkataba wa muda mrefu.

Klabu ya Real Madrid bado wanafuatilia kila kitu kinachoendelea kwenye mazungumzo ya Mbappe na PSG, huku wa
subiri wiki hii iishe
waingie kwenye m
umzo na mchezaji
Klabu ya PSG na
ya wachezaji wa
sha kampeni ya k
mshambuliaji huy
mkataba mpya,
mchezaji Juan Ber
chapisha picha
mtandao wa kijam
na Sergio Ramos,
Herrera, Achraf
na Georginio Wij
wakionyesha jezi
dikwa jina la Mbap
wa na mwaka 2050

LIVE IN PLAY



# SABABU NGUMI KIDUNDA, KATOMPA KUKOSA MBABE

**Na Dennis Fussi**

PAMBANO kati ya Suleiman Kidunda na Erick Tshimanga Katompa kutoka Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC), liliishia raundi ya nne baada ya wawili hao kugongana vichwa katika ukumbi wa Ubungo Plazza Jijini Dar es Salaam usiku wa juzi.

**Wakitumia sheria za WBF baada ya bondia Mtanzania, Kidunda kuchanika juu ya jicho kutokana na kugongwa kichwa na Katompa, mwanzoni mwa raundi ya nne, majaji waliamua kutoa droo.**

Hata hivyo, majaji waliweka wazi hadi pambano hilo la uzito wa middle kuwania ubingwa wa Mabara wa WBF, Kidunda alikuwa anaongoza kwa pointi.

Ikumbukwe, Katompa alimtwanga kwa KO Mtanzania mwingine, Abdallah Shaabani Pazi 'Dullah Mbabe' Oktoba 9, mwaka jana katika ukumbi wa PTA, Temeke jijini Dar es Salaam na jana Kidunda alipewa nafasi kubwa ya kumlipia kisasi Mtanzania mwenzake.

Mapambano mengine ya jana Mtanzania, Ismail Galiatano alishinda kwa pointi dhidi ya Denis Mwale wa Malawi kwenye pambano la nane na kutwaa taji la P.S.T uzito wa Super Bantam.

Mtanzania, mwingine, George Bonabucha alimshinda kwa pointi Mzimbabwe, Hassan Milanzi na kutwaa pia mkanda wa P.S.T, wakati Grace Mwakamele alikuwa Mtanzania pekee aliyepoteza pambano usiku huo baada ya kushindwa kwa pointi na Mmalawi, Ruth Chisale aliyejinyakulia taji la PST pia. Oscar Richard pia alibeba mkanda wa PST baada ya kumtwanga Paul Magesta, Ibrahim C Mgendera 'Ibrah Class alimkalisha Kelvin Majiba kwa Knockout (KO).

Juma Choki alimkalisha kwa KO, Salim Chazama, Vigulo Shafi akamshinda kwa pointi Ally Kilongola na Mwanajeshi mwingine, Haruna Swanga akamshinda Daniel Matefu kwa KO kwenye pambano la tano usiku huo lenye raundi nne.

Iddi Jumanne alimchapa Hamis Kibodi kwa pointi , Joseph Mchapeni alimkalisha Paschal Goba kwa Technical Knockout (TKO) raundi ya pili, Najma Isike akashinda kwa pointi dhidi ya Leila Yazidu na King Makassy alimshinda kwa pointi Ibrahim Mpili.




Mwamuzi akimaliza pambano kati ya Suleiman Kidunda (Kulia) na Erick Tshimanga Katompa na kutangaza matokeo ya sare baada ya kulivunja katika raundi ya nne. **NA MPIGAPICHA WETU**

# *Biashara yakubali muziki wa Yanga*

**Na Dennis Fussi**

MKURUGENZI wa Benchi la Ufundi wa timu ya Biashara United, Madenge Omar, amesema Yanga walistahili ushindi walioupata dhidi yao kwenye mchezo wa Ligi Kuu Tanzania Bara uliochezwa juzi katika Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

Yanga ilitoka nyuma kwa bao 1-0 na kushinda 2-1 dhidi ya Biashara kwenye mchezo uliokuwa na ushindani mkubwa.

Biashara walitangulia kwa bao la Atupele Green Jackson dakika ya kwanza, kabla ya mshambuliaji Fiston Kalala Mayele kuisawazishia Yanga dakika ya 40.

Kiungo mkongwe Mrundi, Said Ntibazonkiza, akaifungia bao la ushindi Yanga dakika ya 79 kwa penalti baada ya beki Abdulmajid Mangaro kumsukuma winga Mkongo, Jeses Moloko.

Akizungumza baada ya mchezo huo, Madenge alisema kwamba, walijua wanacheza na timu kubwa, hivyo ushindi walioupata Yanga walistahili.

"Tuliingia uwajani tukijua tunakwenda kucheza na timu kubwa, hivyo ushindi walioupata wamestahili na kifupi mchezo ulikuwa mzuri sana," alisema Madenge na kuongeza kuwa yeye anaendelea kuwa mkuu wa benchi la ufundi.

Yanga imefikisha pointi 26 katika michezo 10 na kuendelea kuongoza ligi, huku Biashara ikibaki na pointi zake nane za mechi 11 sasa katika nafasi ya 15 kwenye ligi hiyo yenye timu 16.


SPORTPESA APP

BET LEO UWE MILIONEA




MECHI ZA USHINDI

"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE "2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

JUMANNE - 28 - DESEMBA 2021

| TAREHE | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 15:00 | 2814 | Hatayspor vs Menemen Bld | 1.40 | 4.35 | 6.38 |
| 16:00 | 1206 | CR Belouizdad vs USM Alger | 2.20 | 3.05 | 3.65 |
| 16:00 | 5723 | WA Tlemcen vs JS Saoura | 4.10 | 3.05 | 2.06 |
| 16:30 | 4988 | CS Constantine vs NA Hussein Dey | 1.68 | 3.37 | 4.82 |
| 16:30 | 5389 | Paradou AC vs ES Setif | 2.69 | 2.98 | 2.55 |
| 17:00 | 2599 | Hyderabad FC vs Delhi Dynamos FC | 1.50 | 4.24 | 5.01 |
| 17:00 | 5117 | Antalyaspor vs Giresunspor | 2.04 | 3.28 | 3.28 |
| 17:00 | 5818 | Al Wehda vs Alshoulla | 2.07 | 3.10 | 3.90 |
| 18:00 | 1394 | Southend vs Barnet | 2.10 | 3.57 | 3.03 |
| 18:00 | 1537 | Chorley vs Curzon | 1.70 | 3.68 | 4.16 |
| 18:00 | 1765 | Concord Rangers vs Chelmsford | 2.33 | 3.48 | 2.61 |
| 18:00 | 1906 | Hungerford Town vs Chippenham Town | 2.27 | 3.37 | 2.75 |
| 18:00 | 2134 | Altrincham vs Wrexham | 3.56 | 3.46 | 1.94 |
| 18:00 | 2337 | Havant and Waterlooville vs Hemel Hempstead | 1.52 | 4.24 | 4.82 |
| 18:00 | 3110 | Eastleigh vs Torquay | 2.50 | 3.40 | 2.70 |
| 18:00 | 3147 | Crystal Palace vs Norwich City | 1.59 | 3.99 | 5.59 |
| 18:00 | 3202 | Guiseley vs Bradford PA | 2.08 | 3.38 | 3.09 |
| 18:00 | 3607 | Boston Utd vs Brackley Town | 2.16 | 3.29 | 3.00 |
| 18:00 | 3711 | Southampton vs Tottenham | 3.45 | 3.45 | 2.08 |
| 18:00 | 3840 | Leamington vs Telford | 1.83 | 3.52 | 3.71 |
| 18:00 | 3865 | Dagenham and Redbridge vs Aldershot | 1.49 | 4.21 | 5.68 |
| 18:00 | 3876 | MC Alger vs RC Arbaa | 1.35 | 4.04 | 9.05 |
| 18:00 | 3889 | Maidenhead U vs Bromley | 3.66 | 3.66 | 1.86 |
| 18:00 | 4254 | Chesterfield vs Halifax | 1.92 | 3.52 | 3.57 |
| 18:00 | 4324 | Slough Town vs Hampton and Richmond | 3.27 | 3.51 | 1.96 |
| 18:00 | 4558 | Solihull Moors vs Stockport | 3.08 | 3.17 | 2.25 |
| 18:00 | 5251 | Darlington vs Gateshead | 3.65 | 3.51 | 1.85 |
| 18:00 | 5294 | Southport vs Farsley Celtic | 1.34 | 4.72 | 7.12 |
| 18:00 | 5369 | Woking vs Dover | 1.61 | 3.86 | 4.88 |
| 18:00 | 5606 | Blyth Spartans vs Spennymoor Town | 3.22 | 3.61 | 1.95 |
| 18:00 | 5697 | York City vs Alfreton | 2.39 | 3.37 | 2.60 |
| 18:00 | 5726 | Chester vs AFC Fylde | 2.65 | 3.56 | 2.26 |
| 18:00 | 5941 | Braintree vs Dartford | 5.20 | 4.14 | 1.50 |
| 18:00 | 5962 | Maidstone vs Welling | 1.50 | 4.26 | 5.03 |
| 18:00 | 5964 | Watford vs West Ham | 3.35 | 3.50 | 2.10 |
| 18:15 | 5110 | East Riffa vs Manama Club | 2.54 | 3.06 | 2.63 |
| 18:30 | 3258 | Trabzonspor vs Boluspor | 1.29 | 5.03 | 8.12 |
| 18:30 | 5030 | Enppi Club vs Misr Lel Makasa | 1.50 | 3.89 | 6.69 |
| 20:00 | 2261 | MC Oran vs HB Chelghoum Laid | 1.63 | 3.31 | 5.38 |
| 20:00 | 2331 | Tondela vs Gil Vicente | 3.16 | 3.21 | 2.23 |
| 20:30 | 5274 | Muharraq SC vs Riffa Club | 3.36 | 3.31 | 2.00 |
| 20:40 | 1099 | Ahi Nazareth vs Hapoel Raanana | 2.29 | 3.16 | 3.16 |
| 20:40 | 3927 | Ironi Hasharon vs Hapoel Afula | 2.12 | 3.27 | 3.42 |
| 20:40 | 5151 | Hapoel Acre vs AS Ashdod | 3.18 | 2.98 | 2.38 |
| 21:00 | 2603 | CD Feirense vs Benfica Lisbon B | 2.37 | 3.22 | 2.83 |
| 21:00 | 3041 | Talaea El Gaish vs El Gouna | 2.34 | 2.86 | 3.35 |
| 21:00 | 3680 | Galatasaray vs Denizlispor | 1.23 | 5.58 | 9.23 |
| 22:00 | 1657 | Maritimo vs FC Vizela | 2.47 | 3.11 | 2.87 |
| 23:00 | 1847 | Leicester vs Liverpool | 6.61 | 5.41 | 1.38 |
| 23:00 | 3077 | Academica vs CD Trofense | 2.11 | 3.23 | 3.33 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.


o waki-
na wao
nazung-
huyo.
baadhi
meanzi-
umtaka
o asaini
huku
rnat ali-
kwenye
ii akiwa
Ander
Hakimi
naldum
iliyoan-
pe liki-
).

Michezo
Jumanne Desemba 28, 2021
Nipashe



Martial: Nataka kuondoka Man U
UKURASA 21

# Nabi ataja siku ya ubingwa

## ●●● Hata hivyo, akiri mbio bado ni ngumu kwa kila...

**Saada Akida na Adam**

**Fungamwango**

BAADA ya kushuhudia akipata ushindi kwa tabu kwa kutokea nyuma dhidi ya Biashara United kabla ya kushinda 2-1 juzi usiku, Kocha Mkuu wa Yanga, Nasreddine Nabi, amesema anaamini ubingwa wa msimu huu hautakuwa rahisi na bingwa atajulikana siku ya mwisho, hivyo mbinu pekee ya kuubeba ni kupambana hadi dakika za mwisho.

**Nabi alisema hayo juzi baada ya dakika 90 kukamilika kwa mchezo wa Ligi Kuu Tanzania Bara, kwa Yanga kufungua vema maboksi ya zawadi za Krismasi kwa ushindi wa mabao 2-1 katika Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.**

Kocha huyo raia wa Tunisia, alisema mchezo ulikuwa mgumu hasa kwa kuzingatia Biashara United ni moja kati ya timu bora na ndiyo maana iliifunga Al Ahly Tripoli mabao 2-0 kwenye mechi ya Kombe la Shirikisho barani Afrika.

Alisema mchezo ulikuwa wa ufundi zaidi na mgumu na kukiri bao la mapema walilopata Biashara United liliwavuruga sana wachezaji wake, hivyo kuhakikisha wanapambana kusawazisha na kupata ushindi.

"Kufungwa mabao ya mapema ni makosa ya kimpira na wala huwezi kumlaumu yeyote yule, lakini kitendo cha kuanza kufungwa na kuweza kurudisha mpaka kupata ushindi kunaonyesha kuwa Yanga ni timu ya ushindi kwa sababu Biashara United nayo si timu ndogo.

"Wachezaji wangu walipambana, lakini Biashara United walionekana kutafuta sare hali ambayo nilijitoa muhanga kwa kufanya mabadiliko kwa kucheza mabeki watatu badala ya wanne, kuongeza washambuliaji na kupata bao la kusawazisha.

"Baada ya kufanikiwa kusawazisha nilitaka kurudisha mfumo wa kucheza na mabeki wanne, lakini ilishindikana baada ya Shaban Djuma kuumia, wakati nilitaka Dickson Ambundo kuchukua nafasi ya Saido Ntibazonkiza," alisema Nabi.

Alisema mara nyingi timu ikiruhusu bao la mapema, wachezaji wanatumia muda mwingi kurudi mchezoni na nguvu hupungua, lakini wachezaji wake wamepambana na kuweza kuibuka na ushindi.

Yanga ilishtukizwa bao dakika ya pili lililofungwa na Atupele Green, lakini Fiston Mayele na Saido Ntibazonkiza waliipa timu hiyo mabao ya ushindi.

Nabi alisema kiwango kilichoonyeshwa na Biashara United katika mchezo huo kinamfanya kuamini hakuna mechi ambayo itakuwa rahisi huku akidai kwamba bingwa msimu huu atajulikana dakika za mwisho.

"Mara zote nawaeleza wachezaji wangu mechi yoyote mbele yetu ni fainali kwa sababu kila timu imejipanga vizuri na ubingwa msimu huu hautakuwa rahisi na tunatakiwa kupambana hadi dakika za mwisho," alisema Nabi.

Alisema kuhusu maboresho ya kikosi chake kipindi cha dirisha dogo, kwa sasa anahitaji kusajili watu wawili ili kuziba nafasi za wachezaji wagonjwa ambao ni Shomari Kibwana, Yacouba Songne na Abdallah Shaibu 'Ninja'.

"Tunahitaji kupata mtu sahihi ambaye anachukua nafasi ya Yacouba na Shomari Kibwana kwa sababu hao watakuwapo nje kwa muda mrefu," alisema Nabi.

YALAAAH!...



Beki wa Biashara United ya Mara, Abdulmajid Mangalo, akilalama kuchezewa ndivyo sivyo na mshambuliaji wa Yanga, Fiston Mayele, kwenye mechi ya Ligi Kuu Bara iliyopigwa katika Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam juzi na wenyeji kushinda 2-1. **NA MPIGAPICHA WETU**

# Simba kumulika wapinzani CAF leo

**Na Mwandishi Wetu**

WAWAKILISHI pekee wa nchi kwenye michuano ya kimataifa kwa ngazi ya klabu, Simba leo watajua wapinzani wao kwenye hatua ya makundi ya Kombe la Shirikisho Afrika wakati droo itakapochezwa majira ya saa 7:00 mchana jijini Cairo, Misri.

Simba imetinga hatua hiyo ya makundi baada ya kuitoa Red Arrows ya Zambia katika mechi ya mchujo ya michuano hiyo inayoshika nafasi ya pili kwa utajiri kwa ngazi ya klabu barani Afrika.

Mbali na droo hiyo ya Kombe la Shirikisho, pia CAF itachezesha droo ya hatua ya makundi ya Ligi ya Mabingwa Afrika kwa msimu huu wa 2021-22.

Droo hizo mbili Ligi ya Mabingwa na Kombe la Shirikisho, kila moja ina jumla ya timu 16 ambazo zitagawanywa katika makundi manne ya timu nne nne na mechi hatua ya makundi zitaanza kupigwa Februari mwakani.

Timu zilizofuzu hatua ya makundi ya Kombe la Shirikisho Afrika ni Al Ahli Tripoli (Libya), Al Masry (Misri), AS Otoho (Congo), ASEC Mimosas (Ivory Coast), Coton Sport (Cameroon), CS Sfaxien (Tunisia), JS Saoura (Algeria), Orlando Pirates ( Afrika Kusini), Pyramids (Misri), RS Berkane (Morocco), Simba (Tanzania), TP Mazembe (DR Congo), US Gendarmerie Nationale (Niger), Zanaco (Zambia), Al Ittihad (Libya) na JS Kabylie (Algeria) ama Royal Leopards (Eswatini).

Kwa upande wa timu zilizotinga 16-bora Ligi ya Mabingwa ni Al Ahly (Misri), Al Hilal (Sudan), Al Merrikh (Sudan), AmaZulu (Afrika Kusini), CR Belouizdad (Algeria), Esperance (Tunisia), ES Setif (Algeria), Etoile du Sahel (Tunisia), Horoya (Guinea), Jwaneng Galaxy (Botswana), Mamelodi Sundowns (Afrika Kusini), Petro Atletico (Angola), Raja (Morocco), Sagrada Esperanca (Angola), Wydad (Morocco) na Zamalek (Misri).

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >